# Nipashe

Jumamosi Oktoba 31, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580385

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



FURSA

Mawakala na wasambazaji wa uuzaji Magazeti

Kwa Maombi na Ufafanuzi zaidi Wasiliana nasi

Meneja Usambazaji na Masoko
Mikocheni Light Industrial Area
S.L.P 31042,
Dar es Salaam,
Tanzania

Namba :+255716500500

Barua Pepe:circulation@guardian.co.tz

Mwisho wa Maombi ni 27 Oktoba 2020


**ACT-** Wazalendo yadai viongozi wake kutekwa

UKURASA 3



**CCM** yafuta 'uteja' majimbo Kaskazini baada ya miaka 25

UKURASA 3

# Mbunge mteule anusurika kifo

UKURASA 2


## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**WAANGALIZI UCHAGUZI WAVIPA MBINU VYAMA VYA UPINZANI**

TIMU ya waangalizi wa uchaguzi, imevitaka vyama vya siasa vina-vyolalamika kutoridhishwa na...

UKURASA WA 10

**DK. MWINYI APEWA USHAURI ZANZIBAR**

RAIS Mteule wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameshauriwa kuunda serikali itakayokuwa na uwezo wa...


## Vigogo wengine washindwa uchaguzi

UKURASA 3




Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji mstaafu Semistocles Kaijage (kushoto), akijadiliana jambo na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa tume hiyo, Dk. Charles Mahela, wakati wakitangaza matokeo ya awali ya urais katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA MIRAJI MSALA**



# Magufuli azidi kuchanja mbuga matokeo ya urais

- **Awaburuza** wapinzani kwa mbali, Dk. Bashiru ataka wana-CCM wasiwakwaze wengine kwa kushangilia sana... *Endelea ukurasa 2, 5*




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** **SIMBA, YANGA KUJIULIZA BARA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mbunge mteule anusurika kifo nyumba ikichomwa

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MBUNGE Mteule wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi (CCM), amenusurika kifo baada ya nyumba ya familia yake kuchomwa moto na vijana wanaodaiwa wafuasi wa chama cha upinzani.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, alitoa taarifa hiyo jana akifafanua kuwa tukio hilo lilitokea majira ya saa saba usiku wa kuamkia jana nyumbani kwao na Katambi, eneo la Ushirika katika Manispaa ya Shinyanga.

Alisema moto huo ulianza kuwaka juu ya paa la choo cha nje nyumbani kwao na Katambi, mbunge mteule huyo akiwa amelala na ndugu zake.

Kamanda Magiligimba alisema walisikia kishindo kikubwa na walipoamka wakakuta moto unawaka huku pembeni kukiwa na dumu la mafuta ya petroli na baadaye wakaona vijana wawili walionekana wakikimbia na kuingia ndani ya gari.

"Baada ya kufanikiwa kuuzima moto huo, wakaona tena vijana hao wanaingia ndipo wakaanza kulifuatilia gari kwa nyuma, liliingia ndani ya Hospitali ya Rufani mkoani Shinyanga na kisha dereva wa gari hilo kukimbia kwa kuruka ukuta na kufanikiwa kukamatwa vijana wawili ambao walikutwa ndani ya gari," alisema.

Magiligimba alidai gari hilo lilibainika ni la aliyekuwa Mgombea Ubunge wa Shinyanga Mjini (CHADEMA), Salome Makamba, lenye namba za usajili T 729 DFP aina ya Toyota Kullger, ambalo lilikuwa likiendeshwa na mdogo wake aitwaye Timoth Makamba ambaye anadaiwa ndiye aliyeruka ukuta na kukimbia.

Kamanda aliwataja vijana wawili waliokutwa ndani ya gari hilo kuwa ni Wilison Sulutu na Jackson Peter ambao wanadaiwa kuhusika na tukio hilo la kuchoma moto nyumbani kwao na Katambi.

Alisema walikwenda pia nyumbani kwao na Salome Makamba na kufanya upekuzi na kuwakamata vijana wengine wawili ambao ni Justine Owesiga na Gibsoni Mkongwa kwa ajili ya mahojiano zaidi.

Alisema jeshi hilo linaendelea kuwatafuta Makamba pamoja na mdogo wake Timotha, ambao wamekimbilia kusikojulikana.

Alisema jeshi hilo pia linaendelea kufanya uchunguzi juu ya tukio hilo na upelelezi ukikamilika, watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani ili hatua zaidi za kisheria zichukue mkondo wake.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuwapo kwa kundi la watu linalodaiwa kutengeneza njama za kupinga matokeo ya uchaguzi jijini humo.
**PICHA: MIRAJI MSALA**

# Bashiru aonya ushangiliaji CCM

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ali, amewataka wanachama wao kutoshangilia kwa kiwango kikubwa ushindi, ili kuepusha kuwakwaza washindani wao.

Alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na waandishi habari mara baada ya kusali sala ya Ijumaa kwenye Msikiti wa Gadaffi jijini hapa.

Dk. Bashiru alisema ushindi unaopatikana ni wa Watanzania wote wenye kiu na mabadiliko na imani kwa Rais atakayetangazwa. "Matarajio ni kwamba amani iliyotawala wakati wa kampeni na uvumilivu uliotawala, ni mtaji wetu kuwezesha serikali itakayochaguliwa na wabunge watakaochaguliwa kuwa ni serikali ya utumishi na ya maendeleo ya wote," alisema.

Alisema ushindi CCM Zanzibar pia ni Watanzania wote na kwamba Zanzibar ikiimarika na Muungano unaimarika na ikidhoofika na Muungano pia unadhoofika.

"Na sisi katika taifa letu, umoja ni jambo muhimu sana, ushindi uliopatikana ni wa CCM kwa sababu ndiyo utaratibu tulio nao, lakini kusema ukweli wana CCM kama alivyosema Rais mteule wa Zanzibar (Dk. Hussein Mwinyi) tusishangilie sana kuwakwaza washindani wetu. "Ushindi wetu ni ushindi wa Watanzania wote, ni wa umoja wetu, maendeleo yetu na ustawi wetu ni ushindi wa Afrika nzima.

Tusisahau kabisa utulivu katika Tanzania ni utulivu katika Afrika, sisi tunazungukwa na nchi nane, tukipata tatizo hapa, hizi zote nchi nane zinazotutegemea, zitapata tatizo, niwapongeze kwa uamuzi walioufanya," alisema.

Dk. Bashiru pia alimpongeza Dk. Mwinyi kwa ushindi alioupata, akiamini kwamba atakuwa kiongozi wa wote na amedhihirisha hivyo katika kampeni zake.

"Amedhihirisha uungwana wa hali ya juu, uvumilivu wa hali ya juu na uzalendo wa hali ya juu. Tunaimani na matumaini makubwa ahadi zote zilizopo kwenye Ilani upande wa Zanzibar na alizotoa yeye Rais Mteule, tutatekeleza," alisema.

## Waangalizi uchaguzi wavipa mbinu vyama vya upinzani

**Na Beatrice Shayo**

TIMU ya waangalizi wa uchaguzi, imevitaka vyama vya siasa vinavyolalamika kutoridhishwa na mchakato wa uchaguzi mkuu, kuwasilisha malalamiko yao kwa kuzingatia matakwa ya katiba ya nchi na sheria zinazosimamia uchaguzi nchini.

Rais mstaafu wa Burundi na Kiongozi wa Timu ya Waangalizi wa Jumuiya, Sylvestre Ntibantunganya, alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam alipotoa taarifa ya awali ya timu ya watazamaji wa uchaguzi huo kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Alisema timu imepokea taarifa kuwa baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa vilivyoshiriki uchaguzi, wameeleza kutoridhishwa na namna uchaguzi ulivyoendeshwa na mwenendo wa matokeo yanayotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

"Timu inawaomba kuweka mbele maslahi ya Watanzania hususani kuepuka vitendo vyovyote vinavyoweza kusababisha uvunjifu wa amani na utulivu," alisema Ntibantunganya.

Alisema timu ya waangalizi ilitembelea vituo vya kupigakura 160 na kubaini uchaguzi ulifanyika katika mazingira ya amani na utulivu.

Alisema vyama vilivyoshiriki katika uchaguzi pamoja na wagombea wao, waliendesha kampeni zao nchi nzima katika mazingira ya amani na utulivu.

"Vituo vya kupiga kura vilifunguliwa kulingana na matakwa ya sheria na kanuni zinazosimamia uchaguzi," alisema.

Ntibantunganya alisema upigaji kura uliendeshwa kwa uhuru, amani na utulivu.

"Uchaguzi uliandaliwa na kusimamiwa kwa weledi wa hali ya juu. Timu inaipongeza tume kwa namna inavyoendelea kutoa matokea kwa haraka kadri inavyoyoapokea," alisema.

Alisema kulingana na vigezo vya uchaguzi vilivyoainishwa katika mwongozo wa uchaguzi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, uchaguzi huu umekidhi vigezo vyote na ulikua huru na haki.

Alisema timu ya Watazamaji kutoka Jumuiya ya Afrika inawapongeza wananchi wa Tanzania kwa busara waliyoionyesha katika mchakato mzima wa uchaguzi hususani katika kuhakikisha wanadumisha amani na utulivu, jambo ambalo ni muhimu katika mchakato huo.

"Timu inawasihi wananchi wa Tanzania, wagombea nafasi ya urais, ubunge na udiwani kukamilisha hatua zilizobaki za uchaguzi kwa amani na utulivu," alisema.

## CCM yaufuta 'uteja' miaka 25 Kaskazini

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimefanikiwa kushinda katika majimbo ambayo kwa miaka mingi yalikuwa chini ya uwakilishi wa wabunge kutoka vyama vya upinzani.

Kati ya majimbo hayo, yamo Karatu na Moshi Mjini yaliyokuwa yanaongozwa na wabunge wa upinzani kwa miaka 25 iliyopita.

Mbali na majimbo hayo mawili, mengine ya kimkakati yaliyokuwa yakinyemelewa na CCM kwa muda mrefu ni Arusha Mjini, Hai, Vunjo, Mbeya Mjini, Iringa Mjini na Ubungo.

Katika orodha hiyo, yamo majimbo ya kihistoria ambayo CCM ilikuwa inaonekana chama cha upinzani tangu kufanyika kwa uchaguzi wa kwanza uliohusisha mfumo wa vyama vingi mwaka 1995, Moshi Mjini (Kilimanjaro) na Karatu (Arusha) yakiangukia kwenye kundi hilo.

Katika Jimbo la Moshi Mjini ambalo CCM haikuwahi kushinda kwa miaka 25, sasa imelitwaa baada ya Priscus Tarimo kumwangusha hasimu wake wa kisiasa, Raymond Mboya wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Jimbo la Karatu ambalo nalo lina historia inayofanana na Moshi Mjini, nalo limechukuliwa na Daniel Awak wa CCM amelivunja 'uteja', baada ya kumshinda mpinzani wake, Cecilia Pareso (CHADEMA).

CCM imetibua kabisa ngome za upinzani katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini kwa kumng'oa kigogo wa siasa za kiharakati, Godbless Lema (CHADEMA) katika Jimbo la Arusha Mjini. Lema ameliongoza Jimbo la Arusha Mjini kati ya mwaka 2010 na 2015 na baadaye kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka huu. Lema ameangushwa na Mrisho Gambo, aliyewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha.

Jimbo la Hai ambalo lilikuwa liliongozwa kwa miaka 10, kati ya mwaka 2010 na 2015 na mwaka 2015 na 2020 na Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, limechukuliwa na CCM safari hii na kuandika historia mpya katika siasa za Tanzania.

Mbowe ameangushwa katika uchaguzi wa mwaka huu na Saashisha Mafuwe, ambaye kabla ya kuwania kiti hicho cha ubunge, alikuwa Ofisa Utawala wa Tume ya Madini ya Taifa.

Mbeya Mjini nako CCM imemaliza ubishi wa muda mrefu wa kutaka kulitawala jimbo hilo baada ya Dk. Tulia Ackson kumshinda mwanasiasa kijana, msanii mkongwe na mwasisi wa muziki wa kizazi kipya nchini, Joseph Mbilinyi 'Sugu', ambaye amekuwa mbunge wa jimbo hilo kwa miaka 10.

Jimbo la Iringa Mjini ambalo lilikuwa chini ya Mch. Peter Msigwa (CHADEMA) kwa miaka 10, hatimaye limerejea CCM, baada ya Jesca Msambatavangu, mfanyabiashara na Mwenyekiti wa zamani wa chama hicho Mkoa wa Iringa, kumwangusha kutangazwa mshingi katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Katika Jimbo la Vunjo ambalo halina desturi ya kuongozwa na mbunge yeyote kwa miaka zaidi ya mitano, pia limetwaliwa na CCM baada ya kuwa upinzani kwa miaka 15.

Mkurugenzi wa zamani wa Benki ya CRDB, Dk. Charles Kimei, ameshinda ubunge wa jimbo hilo baada ya kumbwaga Mwenyekiti wa Taifa wa NCCR-Mageuzi na Mwenyekiti wa Baraza la Demokrasia Tanzania, James Mbatia.

Jimbo la Ubungo pia limechukuliwa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Dk. Kitila Mkumbo, baada ya kuwapiku kwa kura nyingi wagombea wenzake waliokuwa na nguvu kisiasa, Renatus Pamba wa ACT-Wazalendo na Boniface Jacob (CHADEMA), aliyekuwa Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.

# Vigogo upinzani wazidi kubwagwa

**Na Waandishi Wetu**

BAADA ya matokeo ya juzi kuonyesha vigogo wa upinzani kuangushwa katika majimbo mbalimbali nchini, matokeo yaliyotangazwa jana yalionyesha vigogo wengine wa upinzani kubwagwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Waliokumbwa na baa hilo ni pamoja na aliyekuwa Mbunge wa Vunjo na Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia.

Msimamizi wa uchaguzi wa jimbo hilo, Michael Mwandezi, alitangaza Dk. Charles Kimei kuwa mshindi katika jimbo hilo, akipata upinzani kutoka kwa Grace Kiwelu (Chadema) aliyepata kura 8,675.

Kwa mujibu wa Mwandezi, Mkurugenzi Mkuu wa zamani wa Benki ya CRDB, Dk. Charles Kimei (CCM), amepigiwa kura 40,170.

**GWAJIMA APETA**

Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA), Halima Mdee ameshindwa kutetea kiti cha ubunge Jimbo la Kawe baada ya kuangushwa na mgombea wa CCM, Askofu Josephat Gwajima.

Katika uchaguzi huo ambao matokeo yake yalitangazwa usiku wa kuamkia jana, Askofu Gwajima amepata kura 194,833, wakati Mdee amepigiwa kura 32,524.

Baada ya kutangazwa mshindi, Askofu Gwajima alisema shukrani zake kwa wananchi zitaoneka kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**CCM YAPOTEZA NKASI**

Wakati hali ikiwa ni mbaya kwa vyama vya upinzani, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeanguka katika Jimbo la Nkasi Kaskazini mkoani Rukwa baada ya mgombea wake, Ally Kessy, aliyekuwa anatetea kiti cha ubunge, kupata kura 19, 972 dhidi ya Mgombea wa CHADEMA, Aida Khenan aliyepigiwa kura 21,226.

Hilo lilikuwa jimbo la pili kwa CCM kupoteza Tanzania Bara baada ya juzi, Hawa Ghasia kuangushwa na mgombea wa Chama cha Wananchi (CUF) katika Jimbo la Mtwara Vijijini.

**KARATU**

Katika Jimbo la Karatu, Daniel Awak wa CCM, ameibuka mshindi katika kinyang'anyiro hicho baada ya kupata kura 49,042 dhidi ya mpinzani wake, Cesilia Pareso (CHADEMA) aliyepata kura 31,150.

**MOSHI VIJIJINI**

Aliyekuwa Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Sayansi cha Nelson Mandela cha Jijini Arusha, Profesa Patrick Ndakidemi (CCM), ameshinda kiti cha ubunge wa jimbo hilo.

Profesa Ndakidemi amemwangusha aliyekuwa mbunge wa jimbo hilo kipindi kilichopita, Anthony Komu (CHADEMA), baada ya kupigiwa kura 53,891. Komu aliyehamia NCCR-Mageuzi, ameambulia kura 3,888.

**UBUNGO**

Aliyekuwa Meya wa Dar es Salaam (CHADEMA), Boniface Jacob, ameshindwa katika jimbo hilo na Profesa Kitila Mkumbo (CCM) aliyepata kura 63,221. Jacob amepata kura 20,620.

**■Imeandikwa na Mary Mosha (MOSHI), Allan Isaack (KARATU), Beatrice Moses, Christina Mwakangale (DAR).**



Askari polisi wakiwa wamejazana kwenye gari katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam juzi, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT yadai viongozi wake kutekwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha ACT Wazalendo kimesema bado viongozi wake wanashikiliwa na Jeshi la Polisi akiwamo mgombea wa urais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad.

Maalim Seif aliachiwa kwa dhamana juzi majira ya saa 3:00 usiku kwa mashrti ya kutakiwa kuripoti kituo cha polisi.

Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano wa chama hicho, Salum Bimani, aliwaambia waandishi wa habari jana mjini hapa kuwa viongozi wengine wanaoshikiliwa na polisi ni aliyekuwa mgombea uwakilishi Jimbo la Malindi, Ismail Jussa Ladu.

Aliwataja wengine kuwa ni Makamu Mwenyekiti Juma Duni Haji, Katibu wa Mwenyekiti wa chama hicho, Issa Kheri, aliyekuwa mgombea ubunge jimbo la Shauri Moyo, Maua Muhammed, mgombea mwenza wa chama hicho, Profesa Omar Fakihi.

Bimani alisema Naibu Katibu wa Chama hicho, Nassor Ahmed Mazrui, ametoweka katika mazingira ya kutatanisha na hajulikani alipo mpaka sasa. Alisema kwa mujibu wa taarifa, Mazrui kwa mara ya mwisho alionekana katika Hoteli yake ya Mansson iliyoko jirani na makao makuu ya ofisi za ACT-Wazalendo, Vuga, lakini alitoweka usiku wakati akirejea nyumbani kwake.

"Kuna wanachama na watendaji wetu wa chama wasiopungua 100 Unguja na Pemba wanashikiliwa katika vituo tofauti vya polisi. Wapo waliokamatwa kabla ya kufanyika uchaguzi lakini wanasheria wetu wanaendelea kufuatilia," alisema Bimani.

Alisema Jussa, aliyekuwa mgombea wa Jimbo la Malindi, amelazwa katika Hospitali ya Al-rahma mjini Unguja kutokana na kupigwa na askari juzi walipoandamana kupinga mazingira na mchakato mzima wa uchaguzi mkuu.

Kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa, alisema chama hicho kitatoa msimamo wake iwapo watashiriki au watagomea kama ilivyojitokeza katika serikali iliyopita.

"Bado ni mapema kutoa msimamo wa chama kuhusu Serikali ya Umoja wa Kitaifa lakini hapakuwa na uchaguzi," alisema.

Hata hivyo, alisema hatima ya demokrasia Tanzania ni kuelekea katika mfumo wa chama kimoja kwa sababu CCM imeshindwa kuheshimu misingi ya kidemokrasia na haki za binadamu.

Alisema uchaguzi wa Zanzibar na wa Muungano umefanyika bila kuzingatia misingi ya demokrasia na badala yake kutawaliwa na vitisho vya vyombo vya ulinzi na usalama.

## TCU yafungua dirisha la tatu

**Na Romana Mallya**

TUME ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), imefunga dirisha la pili na kufungua lingine la tatu hadi Novemba 4, mwaka huu, kwa ajili ya udahili wa shahada ya kwanza katika taasisi za elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2020/21.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mtendaji wa tume hiyo, Prof. Charles Kihampa, alisema wamefungua dirisha hilo la udahili baada ya kuwapo na uhitaji zaidi kwa vyuo.

Prof. Kihampa alisema katika awamu zote mbili zilizokamilika jumla ya waombaji 98,935 walituma maombi yao katika vyuo 74 vilivyoidhinishwa kudahili shahada ya kwanza na waliodahiliwa ni 80,792 sawa na asilimia 81.6.

"Waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja ni 41,921 sawa na asilimia 51.8 ya wadahiliwa wote, waliodahiliwa chuo kimoja ni 38,871.

"Wasiodahiliwa katika awamu hizo mbili ni 18,143 ambao wanaruhusiwa kuomba awamu hii ya tatu sambamba na wale ambao hawakufanya hivyo," alisema.

Prof. Kihampa alisema mpaka sasa, waombaji 29,051 sawa na asilimia 69.3 ya waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja, wameshajithibitisha katika chuo kimojawapo.

Alisema baada ya kukamilika awamu hizo mbili, tume ilipokea maombi ya kuongeza muda wa udahili kutoka kwa baadhi ya waombaji waliokosa udahili kutokana na sababu mbalimbali.

Prof. Kihampa alisema TCU ilipokea maombi kutoka Jumuiya ya Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO) na baadhi ya vyuo ambavyo bado vina nafasi katika baadhi ya programu za masomo kwa mwaka wa masomo 2020/21. "Tumefungua awamu ya tatu ya udahili inayoanza leo (jana) hadi Novemba 4 (Jumatano ijayo), ambao hawajapata vyuo tunawaomba watumie fursa hii ili kupata nafasi," alisema.

Pia alisema kwa wale ambao walidahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja kwa awamu zote mbili zilizoisha watumie nafasi hiyo kujithibitisha katika chuo kimojawapo kuanzia jana hadi Novemba 4.

Alisema uthibitisho huo ufanyike kwa kutumia ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri uliotumwa kupitia namba zao za simu au barua pepe walizotumiwa wakati wa kuomba udahili.

Kwa wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo, alisema wanashauriwa kuingia kwenye mfumo wa udahili wa vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kujithibitisha.

Alitaja utaratibu wa udahili awamu ya tatu kwa kuanzia jana hadi Novemba 4, ni kwa ajili ya kutuma maombi ya udahili na kujithibitisha.

# Walioshinda kwa kura nyingi zaidi hawa hapa


Abdulaziz Abood


Angelina Mabula


Askofu Josephat Gwajima


Mrisho Gambo

**Na Romana Mallya**

MATOKEO ya uchaguzi mkuu yametoka yakionyesha upinzani umepoteza karibu majimbo yote dhidi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Wabunge wateule walioshinda kwa kura nyingi zinazoanzia 80,000 ni pamoja Saashisha Mafuwe wa Jimbo la Hai aliyepata kura 89,786 dhidi ya Freeman Mbowe (CHADEMA) aliyepigiwa kura 27,684.

Wengine ni Dk. John Palangyo wa Jimbo la Arumeru Mashariki aliyepata kura 84,858, akifuatwa na Rebeca Mngodo (CHADEMA) kura 14,688.

Wagombea wa CCM walioshinda kwa kura zilizoanzia 100,000 ni pamoja na Ummy Mwalimu katika Jimbo la Tanga Mjini aliyepata kura 114,445 akifuatwa na Mussa Mbarouk wa CUF aliyepigiwa kura 7,497.

Abdul-Aziz Abood wa Jimbo la Morogoro Mjini, pia yumo kwenye orodha hiyo baada ya kushinda kwa kura 171,339 akifuatwa na Devotha Minja (CHADEMA) aliyepata kura 14,139.

Mbunge Mteule wa Kinondoni jijini Dar es Salaam, Abass Tarimba, amepata kura 112,914 akifuatwa na Susan Lyimo (CHADEMA) aliyepata kura 11,260.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi , Dk. Angelina Mabula, pia ameingia kwenye orodha hiyo baada ya kushinda kwa kura 147,724 akifuatwa na Grayson Warrioba (CHADEMA) aliyepata kura 24,022.

Askofu Josephat Gwajima (CCM) pia ametinga katika orodha hiyo baada ya kupata kura 194,833 katika Jimbo la Kawe jijini Dar es Salaam, akimng'oa Halima Mdee wa CHADEMA amepigiwa kura 32,524.

Mrisho Gambo (CCM) amepata kura 82,480 na kumwangusha Godbless Lema (CHADEMA) katika Jimbo la Arusha Mjini. Lema aliyepata kura 46,489 ameliwakilisha jimbo hilo bungeni kwa miaka 10.

Abdallah Chaurembo (CCM) ndiye anashikilia rekodi ya kupigiwa kura nyingi zaidi za ubunge hadi sasa, akishinda kwa kura 280,003 katika Jimbo la Mbagala jijini Dar es Salaam, akifuatwa na Khadija Mwango wa CHADEMA aliyepata kura 13,985.

Waziri wa Nishati, Dk, Medard Kalemani, ameshinda katika Jimbo la Chato mkoani Geita kwa kura 135,999, akifuatwa na Masai Mtabi wa CHADEMA aliyepigiwa kura 7,473.

Boniventura Kiswaga (CCM) amepata kura 136,975 na kushinda kuwakilisha Jimbo la Magu, akifuatwa na Ndindagi Kwizela wa CHADEMA aliyepigiwa kura 14,479.

# Upinzani wapoteza majimbo zaidi

MATOKEO ya uchaguzi mkuu uliofanyika Jumatano, yameendelea kuwa mabaya kwa vyama vya upinzani ambavyo vimepoteza karibu majimbo yote dhidi ya chama tawala, Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Katika matokeo yaliyotangazwa jana, CCM ilianguka katika Jimbo la Nkasi Kaskazini mkoani Rukwa baada ya mgombea wake, Ally Kessy, aliyekuwa anatetea kiti cha ubunge, kupata kura 19, 972 dhidi ya Mgombea wa CHADEMA, Aida Khenan aliyeshinda kwa kura 21,226.

**MUHEZA**

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Hamisi Mwinjuma, maarufu Mwana FA, ameshinda ubunge wa jimbo hilo kwa kura 47,578 dhidi ya mpinzani wake, Yosepher Komba wa CHADEMA aliyepata kura 12,036.

**MASASI MJINI**

Geofrey Mwambe (CCM) ameshinda katika jimbo hilo baada ya kupata kura 17,147, akiafuatwa na mgombea wa CUF aliyepigiwa kura 14,087, Mustafa Swalehe (CHADEMA) aliyepata kura 1,434, Musa Mwadewa wa ACT-Wazalendo kura 536 na Ahmad Nanyohd wa NLD kura 103.

**KARAGWE**

Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, ametetea kiti cha ubunge baada ya kupata kura 68,371 akifuatwa na Adolf Mkono (CHADEMA) aliyepata kura 15,773.

**NGORONGORO**

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, ameshinda katika jimbo hilo kwa kura 63,536, akifuatwa na Jaqueline Swai (CHADEMA) aliyepigiwa kura 7,983 na Olepurko Supeet wa ACT-Wazalendo aliyepata kura 1,080.

**MWANGA**

Katika jimbo hilo, Joseph Thadayo (CCM), ameibuka mshindi kwa kura 27,127, huku mpinzani wake, Hendry Kileo (CHADEMA) akipata kura 4,128, Edward Mfinanga wa NCCR-Mageuzi (866).

**ISMANI**

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ametetea kiti cha ubunge akipata kura 24,934 dhidi ya mgombea wa CHADEMA, Patrick Sosopi aliyepata kura 10,399.

**SAME MASHARIKI**

Anne Kilango Malecela (CCM) ametangazwa mshindi katika jimbo hilo baada ya kupata kura 26,225, huku mpinzani wake, Naghenjwa Kaboyoka (CHADEMA) akipata kura 8,836.

**SAME MAGHARIBI**

David Matayo wa CCM ameshinda kwa kura 24,260, akifuatwa na Gerivas Mgonja wa CHADEMA aliyepata kura 7,558, Majidi Jumanne wa NCC-Mageuzi (200) na Ezekiel Mshigath wa CHAUMMA (133).

**MAJIMBO 10 DODOMA**

Kama ilivyokuwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, CCM imeibuka mshindi kwenye majimbo yote 10 ya Mkoa wa Dodoma. Kati yake, moja (Kongwa) mgombea wa chama hicho, Job Ndugai, ambaye ni Spika wa Bunge, alitangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kupita bila kupingwa.

**KONDOA MJINI**

Ali Makoa wa CCM ameibuka kidedea kwa kupata kura 15,220 huku Mgombea wa CHADEMA, Salehe Kizota, akipata kura 1,862.

**DODOMA MJINI**

Anthony Mavunde, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Vijana), ametetea kiti cha ubunge wa jimbo hilo kwa kura 86,656 dhidi ya mpinzani wake Aisha Kadoga wa CHADEMA ambaye amepata kura 13,589.

**MPWAPWA**

George Malima wa CCM ameibuka mshindi kwa kupata kura 29,693 akifuatiwa na Ezekiel Chisinjila wa CHADEMA ambaye amepata kura 5,989.

**KIBAKWE**

George Simbachawene, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ametetea kiti cha ubunge wa jimbo hilo baada ya kupata kura 37,626, akifuatwa na Msafiri William wa CHADEMA aliyepata kura 5,989.

**CHEMBA**

Mohamed Monni wa CCM ameibuka mshindi kwa kupata kura 35,168. Wagombea wengine na kura zao kwenye mabano ni Kunti Majala wa CHADEMA (21,907), Johnson Gagu wa ACT (1,230), Azizi Abasi wa CHAUMMA (270) na Tanzilu Isema wa CUF (373).

**CHAMWINO**

Deogratius Ndejembi wa CCM ameibuka mshindi kwa kupata kura 67,092 huku mpinzani wake Diana Simba wa CUF akipata kura 990.

**BAHI**

Mgombea Keneth Nollo (CCM), ameibuka kidedea kwa kupata kura 40,629 akifuatiwa na Mgombea wa CUF, Godfrey Pamwe, aliyepata kura 2,254.

**KONDOA VIJIJINI**

Dk. Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, ametetea kiti cha ubunge wa jimbo hilo kwa kura 38,131. Wagombea wengine na kura zao kwenye mabano ni pamoja na Monica Safari wa CHADEMA (5,688), Hadija Issa wa CUF (4,738) na Said Njuki wa ACT-Wazalendo (1,033).

**MVUMI**

Livingstone Lusinde wa CCM ametetea ubunge wa jimbo hilo kwa kupata kura 41,371 huku wapinzani wake Hadija Maula wa CHADEMA na Daudi Msanjila wa CUF wakipata kura 5,665 na 302, mtawalia.

**•Imeandikwa na Hamisi Nasri (MSASI), Allan Isaack, (NGORONGORO), Mary Mosha (SAME), Godfrey Mushi (MWANGA) na Augusta Njoji (DODOMA)**

# JPM azidi kuchanja mbuga urais

**Na Mary Geofrey**

MGOMBEA Urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli (pichani), ameendelea kuongoza katika kura kutokana na uchaguzi uliofanyika Jumatano wiki hii dhidi ya wagombea wengine 16.

Katika matokeo yanayoendelea kutangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi NEC, Dk. Magufuli ambaye anawania muhula wa pili wa urais, hadi jana jioni, alikuwa anaongoza huku akifuatiwa kwa mbali na Tundu Lissu wa Chama cha Maendeleo na Demokrasia (CHADEMA).

Hadi wakati huo, NEC ilikuwa imetangaza matokeo kutoka majimbo 231 ya uchaguzi kati ya 264 huku Dk. Magufuli akiwa na asilimia 84.96 na Lissu asilimia 12.39. Mgombea wa ACT Wazalendo, Bernard Membe, alikuwa anashika nafassi ya tatu kwa asilimia 0.57 na Leonard Mahona wa NRA asilimia 0.54.



**Matokeo ya kura za urais kutoka katika baadhi ya majimbo ni kama ifuatavyo;-**

**SINGIDA MAGHARIBI**
John Magufuli (CCM) 35,012 Leopard Mahona (NRA) 343, John Shibuda (ADA TADEA) 91, Muttamwega Mgaywa (SAU) 45, Cecilia Mwanga (Demokrasia Makini) 45, Yeremia Maganja (NCCR-Mageuzi) 41, Ibrahim Lipumba (CUF) 60 , Philipo Fumbo (DP) 18, Bernard Membe (ACT-Wazalendo) 41 na Queen Sendiga (ADC) 9.
Wengine ni Twalib Kadege (UPDP) 16, Hashim Rungwe (CHAUMMA) 99, Khalfan Mazrui (UMD) 9, Seif Seif (AAFP) 8 na Tundu Lissu (CHADEMA) 6,218.

**SINGIDA MASHARIKI**
Magufuli (26,422), Mahona (284), Shibuda (252), Muttamwega (84), Mwanga (111), Maganja (112), Lipumba (99), Fumbo (37), Membe (51), Sendiga (9), Kadege (20), Rungwe (353), Mazrui (8), Seif (11) na Lissu (17,228).

**KAHAMA MJINI**
Magufuli (167,480), Mahona (42), Shibuda (55), Muttamwega (38), Mwanga (48), Maganja (479), Lipumba (1,391), Fumbo (58), Membe (1,143), Sendiga (25), Kadege (50), Rungwe (196), Mazrui (23), Seif (27) na Lissu (9,512).

**KIBAHA MJINI**
Magufuli (37,323), Mahona (94), Shibuda (50), Muttamwega (22), Mwanga (29), Maganja (48), Lipumba (127), Fumbo (17), Membe (37), Sendiga (13), Kadege (16), Rungwe (170), Mazrui (5), Seif (8) na Lissu (6,777).

**KONDE**
Magufuli (1,786), Mahona (26), Shibuda (33), Muttamwega (16), Mwanga (9), Maganja (14), Lipumba (98), Fumbo (6), Membe (681), Sendiga (24), Kadege (17), Rungwe (42), Mazrui (5), Seif (8) na Lissu (2,329).

**KUSINI PEMBA**
Magufuli (2,945), Mahona (39), Shibuda (57), Muttamwega (22), Mwanga (12), Maganja (35), Lipumba (53), Fumbo (21), Membe (677). Sendiga (58), Kadege (33), Rungwe (50), Mazrui (15), Seif (19) na Lissu (1,703).

**BAGAMOYO**
Magufuli (26,203), Mahona (184), Shibuda (95), Muttamwega (30), Mwanga (26), Maganja (37), Lipumba (366), Fumbo (16), Membe (245), Sendiga (17), Kadege (16), Rungwe (113), Mazrui (5), Seif (5) na Lissu (5,010).

**LONGIDO**
Magufuli (64,928), Mahona (83), Shibuda (10), Muttamwega (8), Mwanga (5), Maganja (5), Lipumba (6), Fumbo (0), Membe (0), Sendiga (4), Kadege (2), Rungwe (7), Mazrui (2), Seif (2) na Lissu (1,177).

**BUMBULI**
Magufuli (46,745), Mahona (341), Shibuda (133). Muttamwega (41), Mwanga (31), Maganja (66), Lipumba (20), Fumbo (43), Membe (32), Sendiga (33), Kadege (21), Rungwe (73), Mazrui (8), Seif (9) na Lissu (2,373)

**KIEMBE SAMAKI**
Dk. Magufuli (10,881), Mahona (19), Shibuda (17), Muttamwega (15), Mwanga (6), Maganja (18), Lipumba (32), Fumbo (6), Membe (681), Sendiga (28), Kadege (8), Rungwe (22), Mazrui (4), Seif (5) na Lissu (1,402).

**DIMANI**
Magufuli (13,595), Mahona (34), Shibuda (23), Muttamwega (16), Mwanga (20), Maganja (25), Lipumba (83), Fumbo (12), Membe (883), Sendiga (18), Kadege (8), Rungwe (45), Mazrui (10), Seif (7) na Lissu (1,172).

**FUONI**
Magufuli (7,843), Mahona (34), Shibuda (27), Muttamwega (3), Mwanga (10), Maganja (4), Lipumba (40), Fumbo (6), Membe (391), Sendiga (5), Kadege (4), Rungwe (21), Mazrui (4), Seif (2) na Lissu (458).

**PANGAWE**
Magufuli (8,141), Mahona (22), Shibuda (ADA TADEA) 31, Muttamwega (17), Mwanga (13), Yeremia (19), Lipumba (111), Fumbo (13), Membe (1,132), Sendiga (38), Kadege (12), Rungwe (49), Mazrui (7), Seif (10) na Lissu (1,567.)

**GEITA MJINI**
Magufuli (48,890), Mahona (455), Shibuda (224), Muttamwega (32), Mwanga (51), Maganja (67), Lipumba (68), Fumbo (42), Membe (42), Sendiga (10), Kadege (23), Rungwe (194), Mazrui (13), Seif (13) na Lissu (9,488).

**NEWALA VIJIJINI**
Magufuli (23,424), Mahona (424), Shibuda (281), Muttamwega (100), Mwanga (68), Maganja (67), Lipumba (1,623), Fumbo (71), Membe (481), Sendiga (22), Kadege (61) Rungwe (126), Mazrui (17), Seif (39) na Lissu (10,725).

**MTWARA VIJIJINI**
Magufuli (34,446), Mahona (445), Shibuda (190), Muttamwega (248), Mwanga (90), Maganja (138), Lipumba (4,286), Fumbo (78), Membe (174), Sendiga (37), Kadege (48), Rungwe (181), Mazrui (62), Seif (32) na Lissu (6,879).

**KIGAMBONI**
Magufuli (39,177), Mahona (143), Shibuda (73), Muttamwega (44), Mwanga (50), Maganja (54), Lipumba (276), Fumbo (32), Membe (214), Sendiga (28), Kadege (11), Rungwe (253), Mazrui (4), Seif (21) na Lissu (9,571).

**MUHAMBWE**
Magufuli (38,213), Mahona (627), Shibuda (280), Muttamwega (21), Mwanga (66), Maganja (169), Lipumba (101), Fumbo (46), Membe (183), Sendiga (32), Kadege (35), Rungwe (137), Mazrui (14), Seif (17) na Lissu (8,621).

**MPANDA VIJIJINI**
Magufuli (38,245), Mahona (270), Shibuda (88), Muttamwega (51), Mwanga (45), Maganja (25), Lipumba (35), Fumbo (17), Membe (80), Sendiga (5), Kadege (10), Rungwe (73), Mazrui (6), Seif (5) na Lissu (4,860).

**MKINGA**
Magufuli (27,699), Mahona (293), Shibuda (164), Muttamwega (105), Mwanga (58), Maganja (82), Lipumba (2,501), Fumbo (50), Membe (255), Sendiga (33), Kadege (37, Hashim Rungwe (CHAUMMA) 86, Khalfan Mazrui (UMD) 31, Seif Seif (AAFP) 23 na Tundu Lissu (CHADEMA) 3,609.

**MANYONI MAGHARIBI**
John Magufuli (CCM) 20,130, Leopard Mahona (NRA) 254, John Shibuda (ADA TADEA) 94, Muttamwega Mgaywa (SAU) 30, Cecilia Mwanga (Demokrasia Makini) 19, Yeremia Maganja (NCCR-Mageuzi) 19, Ibrahim Lipumba (CUF) 23, Philipo Fumbo (DP) 12, Bernard Membe (ACT-Wazalendo) 19 na Queen Sendiga (ADC) 9.
Twalib Kadege (UPDP) 11, Hashim Rungwe (CHAUMMA) 72, Khalfan Mazrui (UMD) 5, Seif Seif (AAFP) 31 na Tundu Lissu (CHADEMA) 3,923.

**MWIBARA**
John Magufuli (CCM) 23,430, Leopard Mahona (NRA) 464, John Shibuda (ADA TADEA) 159, Muttamwega Mgaywa (SAU) 174, Cecilia Mwanga (Demokrasia Makini) 61, Yeremia Maganja (NCCR-Mageuzi) 92, Ibrahim Lipumba (CUF) 37, Philipo Fumbo (DP) 27, Bernard Membe (ACT-Wazalendo) 41 na Queen Sendiga (ADC) 9.
Wengine ni Twalib Kadege (UPDP) 26, Hashim Rungwe (CHAUMMA) 148, Khalfan Mazrui (UMD) 9, Seif Seif (AAFP) 26 na Tundu Lissu (CHADEMA) 6,172.

**MFENESINI**
John Magufuli (CCM) 10,313, Leopard Mahona (NRA) 69, John Shibuda (ADA TADEA) 50, Muttamwega Mgaywa (SAU) 20, Cecilia Mwanga (Demokrasia Makini) 10, Yeremia Maganja (NCCR-Mageuzi) 11, Ibrahim Lipumba (CUF) 68, Philipo Fumbo (DP) 9, Bernard Membe (ACT-Wazalendo) 604 na Queen Sendiga (ADC) 52.
Wengine ni Twalib Kadege (UPDP) 14, Hashim Rungwe (CHAUMMA) 31, Khalfan Mazrui (UMD) 5, Seif Seif (AAFP) 4 na Tundu Lissu (CHADEMA) 946.

**WINGI (UNGUJA KASKAZINI)**
John Magufuli (CCM) 2,695, Leopard Mahona (NRA) 60, John Shibuda (ADA TADEA) 23, Muttamwega Mgaywa (SAU) 24, Cecilia Mwanga (Demokrasia Makini) 13, Yeremia Maganja (NCCR-Mageuzi) 29, Ibrahim Lipumba (CUF) 49, Philipo Fumbo (DP) 10, Bernard Membe (ACT-Wazalendo) 732, na Queen Sendiga (ADC) 42.
Wengine ni Twalib Kadege (UPDP) 14, Hashim Rungwe (CHAUMMA) 40, Khalfan Mazrui (UMD) 14, Seif Seif (AAFP) 51 na Tundu Lissu (CHADEMA) 1,006.

**MAGOMENI**
John Magufuli (CCM) 7,571, Leopard Mahona (NRA) 16, John Shibuda (ADA TADEA) 15, Muttamwega Mgaywa (SAU) 4, Cecilia Mwanga (Demokrasia Makini) 16, Yeremia Maganja (NCCR-Mageuzi) 23, Ibrahim Lipumba (CUF) 45, Philipo Fumbo (DP) 12, Bernard Membe (ACT-Wazalendo) 728, na Queen Sendiga (ADC) 31.
Wengine ni Twalib Kadege (UPDP) 13, Hashim Rungwe (CHAUMMA) 32, Khalfan Mazrui (UMD) 6, Seif Seif (AAFP) 3 na Tundu Lissu (CHADEMA) 1,247.

**BUYUNGU**
John Magufuli (CCM) 30899, Leopard Mahona (NRA) 321, John Shibuda (ADA TADEA) 149, Muttamwega Mgaywa (SAU) 128, Cecilia Mwanga (Demokrasia Makini) 101, Yeremia Maganja (NCCR-Mageuzi) 104, Ibrahim Lipumba (CUF) 38, Philipo Fumbo (DP) 28, Bernard Membe (ACT-Wazalendo) 68 na Queen Sendiga (ADC) 2.
Wengine ni Twalib Kadege (UPDP) 24, Hashim Rungwe (CHAUMMA) 126, Khalfan Mazrui (UMD) 17, Seif Seif (AAFP) 19, Tundu Lissu (CHADEMA) 9694.

**RUFIJI**
John Magufuli (CCM) 25140, Leopard Mahona (NRA) 306, John Shibuda (ADA TADEA) 144, Muttamwega Mgaywa (SAU) 79, Cecilia Mwanga (Demokrasia Makini) 48, Yeremia Maganja (NCCR-Mageuzi) 69, Ibrahim Lipumba (CUF) 1313, Philipo Fumbo (DP) 37, Bernard Membe (ACT-Wazalendo) 655, na Queen Sendiga (ADC) 28.
Wengine ni Twalib Kadege (UPDP) 40, Hashim Rungwe (CHAUMMA) 85, Khalfan Mazrui (UMD) 16, Seif Seif (AAFP) 11, Tundu Lissu (CHADEMA) 3886.

**MULEBA KASKAZINI**
John Magufuli (CCM) 39,446, Leopard Mahona (NRA) 419, John Shibuda (ADA TADEA) 130, Muttamwega Mgaywa (SAU) 37, Cecilia Mwanga (Demokrasia Makini) 50, Yeremia Maganja (NCCR-Mageuzi) 71, Ibrahim Lipumba (CUF) 32, Philipo Fumbo (DP) 19, Bernard Membe (ACT-Wazalendo) 43 na Queen Sendiga (ADC) 11.
Wengine ni Twalib Kadege (UPDP) 16, Hashim Rungwe (CHAUMMA) 108, Khalfan Mazrui (UMD) 4, Seif Seif (AAFP) 49, Tundu Lissu (CHADEMA) 8037.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi Ligi Kuu Bara ongezeni umakini, haki

**LIGI** Kuu Bara ambayo msimu huu inashirikisha timu 18 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini, ndio ligi ya juu inayotegemewa kutoa wachezaji wengi wanaounda kikosi cha Timu ya Taifa ya Tanzania maarufu Taifa Stars.

Pia ndio ligi inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, inayofanyika kila mwaka barani hapa.

Kwa msimu mpya wa mashindano hayo ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), utakaoanza baadaye mwezi ujao, mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Simba na Namungo ya Lindi, ndio watakwenda kupeperusha bendera ya nchi kwenye michuano hiyo, pamoja na Mlandege na JKU kutoka Zanzibar.

Ili kupeleka wawakilishi ambao wameiva, wameimarika na wako tayari kupambana kusaka ushindi, ni lazima timu hizo ziwe zimepitia katika maamuzi sahihi ya marefa wa hapa nchini.

Marefa wanapofanya majukumu yao kwa kuchezesha kwa haki, umakini na kufuata sheria 17 za soka, timu zinazopata ushindi zinakuwa zimepita kwenye misingi sahihi na si kwa njia ya 'makandokando'. Endapo waamuzi watachezesha mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kiwango cha juu, itakuwa ni faida kwa wachezaji ambao hawataona wanaonewa pale watakapokwenda kwenye mashindano ya kimataifa.

Mchezaji ambaye amezoea 'kubebwa' na waamuzi wa hapa nchini, huwa kwenye wakati mgumu anapokuwa katika mashindano ya kimataifa hivyo, huifanya timu yake kusaka ushindi kwa shida na hivyo hujikuta wanatolewa mapema katika michuano wanayoshiriki.

Mbali na Bodi ya Ligi kutoa adhabu kwa waamuzi ambao wanachezesha chini ya kiwango kwa kushindwa kutafsiri vyema sheria za mchezo huo, uamuzi huo pekee hautatosha kumaliza tatizo.

Mwamuzi atafungiwa kwa muda kadhaa au ataondolewa kwenye orodha ya waamuzi kwa msimu husika, lakini maumivu ya timu ambayo ilistahili ushindi au kwa maneno mengine ilionewa katika mchezo husika yataendelea kuwa kovu kwenye mioyo ya timu husika.

Lakini pia itapunguza hamasa ya mashabiki wanaojitokeza uwanjani kushangilia timu zao kwa kuendelea kuona waamuzi wanaboronga kwenye kazi yao. Umefika wakati waamuzi wakaongeza umakini na weledi katika majukumu ambayo wanakabidhiwa ili mwisho wa msimu, bingwa anayestahili apatikane na kwenda kupeperusha vyema bendera ya Tanzania kwenye mashindano ya kimataifa.

Nipashe inawakumbusha waamuzi kuitendea vyema taaluma yao kwa sababu imekuwa ikiwaingizia kipato cha kuendesha familia zao kama zilivyo taaluma nyingine, hivyo kuongeza umakini kutawasaidia kuimarisha viwango vyao na hatimaye kuteuliwa kwenye mechi za kimataifa.

Tujiulize, kwa nini Tanzania imekuwa haipeleki waamuzi kwenye mashindano ya kimataifa? Jibu ni moja, waamuzi wetu wamekuwa na viwango vya chini na hivyo wanatakiwa kujijenga upya na hatimaye kujifungulia njia ya kuteuliwa na CAF katika michuano yake.

Adhabu ya kuwafungia waamuzi haitaweza kubadilisha viwango vyao, lakini ni vyema Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), likaongeza madarasa ya kuwanoa marefa hao kwa malengo ya kuwakumbusha kutekeleza vizuri majukumu yao na kuacha utaratibu wa kuwafundisha kwa awamu moja ya kabla ya kuanza kwa msimu.


Wakati waamuzi wakitakiwa kurejea katika mstari, wachezaji wote mnakumbushwa kuzingatia nidhamu katika michezo yote ya ligi na ya kimataifa.

Nidhamu ya mchezaji husaidia kuondoa purukushani mbalimbali katika mechi husika, na hiyo itamfanya mwamuzi kuwa na kazi nyepesi ya kutekeleza majukumu yake na hatimaye baada ya dakika 90 kumalizika, timu iliyostahili kupata ushindi iondoke na pointi zote au zigawane pointi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Mvua inyeshe leo ...

**"MVUA** inyeshe leo na uyoga upate leo?" Haiwezekani mvua kunyesha leo na mtu kupata uyoga (mmea jamii ya kuvu*) leo.

Methali ya mvua hutumiwa kumshauri mtu asiwe na pupa afanyapo jambo. Tunapaswa kuwa na subira kwa mambo tufanyayo.

Husemwa "mvumilivu hula mbivu" kwani anayevumilia hula kilichoiva. Tunasihiwa tuwe na subira tutakapo mafanikio kwani "haraka haraka haina Baraka," chambilecho (kwa mujibu wa) wahenga.

'Mauzauza' ni hali ya macho kudanganyika na kuyafanya yaone kitu ambacho sivyo kilivyo; ukosefu wa fahamu timamu (kuwa makini katika kufanya jambo) unaosababishwa na hali kama ulevi au kutoka usingizini. Tembelea masoko yanayouza matunda ya aina mbalimbali kisha uliza ubora wake: "Matunda haya ni mazuri?" Utajibiwa: "ni mazuri sana ..." Kama hujui ghiliba (udanganyifu wenye nia ya kujinufaisha) za wauza matunda, utanunua haraka.

Mbivu na mbovu utajua ukifika nyumbani kuwa ulivyoambiwa na kuhakikishiwa ubora wa matunda uliyonunua ni tofauti kama maji na mafuta!

Ukisoma kurasa za mbele za magazeti yetu ya michezo, utavutiwa na vichwa mbalimbali vya habari, hasa zinazohusu Simba na Yanga. Hata kama hukutaka kununua ilhali wewe ni shabiki au mwanachama wa moja ya vilabu husika, utanunua tu.

Unapofika nyumbani na kuanza kusoma utaona tofauti kuubwa kati ya yaliyoandikwa kurasa za mbele na yaliyoandikwa kwa kirefu kurasa za ndani!

Kabla Yanga haijapambana na 'wenyeji' wao, KMC ya Kinondoni, iliandikwa hivi kwenye ukurasa wa mbele wa gazeti la michezo: "Yanga SC yapindua matokeo Mwanza."

Je, mwandishi alikuwa na maana ya kulinganisha mapokezi ya KMC walioitangulia Yanga kufika Mwanza kwa namna walivyopokewa?

Timu hizo zilipocheza, kesho yake gazeti hilo liliandika kwenye ukurasa wake wa mbele kwa herufi kubwa: "MAVITU YA KAZE ... YANGA HADI RAHA."

Kitabu cha 'Methali na Mawaidha' kilichoandikwa na Mathias E. Mnyampala (Mungu amrehemu) chaeleza kuwa: "Akataaye kuonywa mara nyingine) roho yake; lakini asikiaye akikanywa hujipatia akili zaidi."

Turejelee (pitia jambo au kitu kwa mara nyingine) kichwa cha habari kwenye gazeti la michezo lilivyoandika kuhusu mechi kati ya KMC na Yanga iliyochezwa tarehe 25 Oktoba, 2020 na Yanga kushinda kwa mabao 2-1.

Kichwa cha habari kiliandikwa kwa herufi kubwa kama nilivyonakili huko juu kuwa: "Mavitu ya Kaze ... Yanga hadi raha."

'Mavitu' maana yake nini? Twajua kuwa 'kitu' ni chochote kinachoweza kubainishwa kwa kutumia milango ya fahamu kama vile kuonekana, kushikika, kuonjwa n.k. Wingi wa 'kitu' ni 'vitu' si 'mavitu' kama ilivyoandikwa na gazeti ninalolikosoa.

'Raha' ya mwandishi ni goli la kusawazisha walilofunga Yanga kwa penalti yenye utata?

Husemwa "Msema kweli hakosi." Maana yake mtu asemaye ukweli hakosi kwani asemalo huwa. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kwamba aghalabu mtu mwenye tabia ya kusema kweli huishia kuaminiwa na watu wengine. Ni vizuri tuwe na tabia ya kusema kweli ndipo tuaminiwe.

Mwalimu Kaze kaikuta Yanga ikiwa haina mchezo unaovutia na ushindi wake ni wa kubahatisha kwa kufunga bao moja moja tena kwa mbinde (taabu kubwa katika kufanya jambo).

Kumlaumu au kum-beza Kaze ni kumwonea kwani amekuwa na timu ya Yanga kwa kipindi kifupi sana kuweza kuibadili.

Ilivyoandikwa na gazetini baada ya Yanga kupata 'ushindi' wa mabao 2-1 dhidi ya KMC jijini Mwanza: "Gari ndio limewaka. Shughuli ya Kaze imeleta mzuka kwa mabosi na mastaa wa klabu hiyo na sasa ...Kaze anatisha staili ya gusa achia moto, wafichua matatizo."

Hiyo staili ya 'gusa achia' niliiona kwa KMC iliyowafanya wachezaji wa Yanga wacheze kama wanaofundishwa namna ya kujipanga na kupeana pasi zinazofika maeneo yaliyokusudiwa. Walikimbizwa tu uwanjani kama wanafunzi!

Kumsifu kocha Kaze ambaye hajakaa na timu kwa muda mrefu ni kumdhihaki, yaani kumpa sifa za uongo; kumtania. Tangu aanze kuifundisha Yanga hajamaliza hata mwezi mmoja. Leo kupewa kongole (shukrani) ni unafiki!

Kaze apewe muda wa kutosha ili kuifanya timu icheze mchezo unaofurahisha watazamaji na kupata ushindi wa mabao mengi, sio bao moja moja tena kwa mbinde!

Ilipocheza na KMC kule Mwanza tuliona ilivyohangaishwa na kufungwa bao la utangulizi mpaka Yanga ilipopewa penalti yenye shaka.

Ulaya wana Kamati za Waamuzi kulingana na nchi husika na mashindano husika. Waamuzi wanapokuwa uwanjani hufanya kazi kwa msaada wa chombo kinachoitwa VAR.

Kunapokuwa na ubishi wa bao lililofungwa au kukataliwa ama penalti kukataliwa au kukubaliwa na mwamuzi, VAR huwa mwamuzi sahihi.




Mkuu wa Wilaya ya Karatu, mkoani Arusha, Abbas Kayanda (kulia), akikabidhi fedha zaidi ya Sh. milioni 2.2 za ofisi ya kijiji Mbulumbulu kwa Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Faraja Msigwa, zilizookolewa na Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa nchini (TAKUKURU), baada ya kufanyiwa ubadhilifu na uongozi wa kijiji hicho. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Tanzania, Uganda zatia saini utekelezaji bomba la mafuta

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

SERIKALI ya Tanzania imetia saini makubaliano ya awali ya utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kati yake na Kampuni ya Total East Africa.

Bomba hilo linalojengwa kutoka Kijiji cha Chongoleani mkoani Tanga hadi Hoima nchini Uganda, litagharimu Dola za Marekani bilioni 3.5, sawa na Sh. trilioni nane za Tanzania.

Jana, Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Prof. Adelardius Kilangi, akizungumza baada ya kutiliana saini makubaliano hayo, alisema majadiliano kuhusu kuendelea kwa mradi huo yamechukua takribani wiki tatu, huku nchini Uganda yakichukua miezi mitatu.

Prof. Kilangi alisema awali Rais wa Uganda, Yoweri Mseveni, alikutana na Rais John Magufuli nyumbani kwake Chato mkoani Geita, Septemba 13, mwaka huu, na kukubaliana kila nchi ifanye makubaliano ya haraka na upande wa mradi wa EACOP ili mchakato wake uanze mara moja.

Alisema makubaliano hayo yamezingatia, haki ya ardhi, matumizi ya rasilimali za ndani, masuala ya afya na usalama, mazingira pamoja na viwango vya ajira.

"Bomba hilo ambalo lina urefu wa kilomita 900, mchakato wake unapaswa kukamilika ndani ya miezi minne au mitano ijayo, na mradi unatarajiwa kuanza rasmi Februari mwaka ujao," alisema Dk. Kilangi

Kwa mujibu wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, faida za uwekezaji wa mradi huo ni pamoja na ajira 10,000 kwa Watanzania, mapato ya kodi, ujenzi wa barabara na miundombinu mbalimbali na ujenzi wa bandari mpya.

Faida nyingine ni pamoja na upatikanaji wa fursa mbalimbali za kibiashara, usafirishaji, ulinzi, chakula na vinywaji na mahoteli kwa ajili ya malazi.

Aidha, alieleza zaidi kuwa mradi huo ni kielelezo muhimu cha kupokea uwekezaji mkubwa na kuwakaribisha wawekezaji wengine kuja kuwekeza nchini kutokana na mazingira mazuri ya uwekezaji.

Awali, Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (TPSF), Angelina Ngalula alimpongeza Rais Magufuli na Rais Museveni kwa hatua ya kuingia mkataba wa makubaliano hayo, kwa kuwa wafanyabiashara wa Tanzania, kwao ni fursa tosha ya kuzalisha mabilioni ya fedha.

## Serikali yarejesha mil. 19.5/- vitambulisho vya wajasiriamali

**Na Woinde Shizza,** KARATU

SERIKALI imesema imerejesha katika mikono yake, Sh. milioni 19.5 za vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga, baada ya kupotea katika mazingira ya kutatanisha.

Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Abbas Kayanda, amesema kupatikana kwa fedha hizo zilizokuwa zimechukuliwa na wajanja wachache, kumetokana na serikali kujikita kupambana na rushwa na kusimamia haki.

Kayanda alikuwa akizungumza jana, wakati wa hafla fupi ya makabidhiano ya fedha hizo kati yake na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu.

"Hizi pesa ni za vitambulisho vya machinga vilivyokuwa vimetolewa awamu ya kwanza. Wajanja wakapita nazo na sisi tukaiagiza TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) kuingia kazini, kufanyia kazi taarifa ya kuwapo kwa ubadhirifu wa fedha hizo.

"Lakini niwaonye tena watumishi wetu wa umma kwamba vitendo vya namna hii ni vitendo ambavyo havifai na vinaweza kumfanya mtumishi afukuzwe kazi. Muwe makini," alisema.

Inaelezwa kuwa vitambulisho hivyo vya awali havikuwa na alama yoyote ya mhusika, hivyo kutoa mwanya kwa waliopewa kupeana bila utaratibu.

Mkuu huyo wa wilaya, alitoa rai kwa watendaji vijiji kuheshimu fedha ambazo serikali inaleta kwa ajili ya miradi ya maendeleo, lakini kuheshimu fedha ambazo wananchi wanachangia kwa ajili ya miradi ya maendeleo, fedha hizo lazima zitumike kwa kufuata utaratibu wa serikali.

Vitambulisho vya machinga vilitolewa kwa mara ya kwanza Disemba 10, 2018 na Rais John Magufuli, akisema kila atakayekuwa na kitambulisho cha aina hiyo asibughudhiwe katika eneo atakalokuwa akifanyia shughuli zake.

Rais Magufuli aliamua kutoa vitambulisho hivyo, baada ya serikali za mikoa na wilaya kushindwa kumpa utaratibu wa jinsi wafanyabiashara hao wadogo wanavyoweza kufanya kazi katika mazingira yasiyo na bughudha.

## RC ataka kitengo kubaini mikopo umiza wananchi

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Singida kwa kushirikiana na vyombo vyote vya dola, kuanzisha kitengo cha uchunguzi kuwatambua wakopeshaji umiza walioko mkoani hapa.

Dk. Nchimbi alitoa agizo hilo jana kwenye ukumbi wa mikutano wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa, alipokuwa akipokea taarifa ya fedha zilizookolewa na TAKUKURU Mkoa wa Singida kutokana na riba umiza kwa kipindi cha Julai hadi Oktoba, mwaka huu.

Mkuu wa Mkoa huyo alisisitiza kwamba wakati umefika sasa wa serikali kuwafuatilia wakopeshaji umiza wote na kuwatambua mahali walipo na nini wanachofanya na taarifa zao zitunzwe katika dawati la siri.

"Ufuatiliaji huo usiangalie kama mkopeshaji huyo ameshawahi kushtakiwa au hajawahi kushtakiwa. Wawe wamekuja kulalamikiwa au hawajalalamikiwa kwa sababu tutakuwa tunawafahamu. Tutawachimba na kuwachimbua kisawasawa," alisema.

Dk. Nchimbi ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya mkoa, alitumia fursa ya kikao hicho kwa kuwapongeza baadhi ya wakopeshaji umiza ambao baada ya agizo hilo na kwa kumtanguliza Mungu, wakafikia uamuzi ya kujisalimisha mapema.

"Ndugu zangu kukopa si dhambi, kukopeshana si dhambi lakini dhambi iko katika kutokufuata taratibu. nchi yetu ni taratibu na sheria na ingekuwa si kufuata taratibu na sheria, Tanzania isingekuwa hivi," alisisitiza huku akiwakodolea baadhi ya wakopeshaji umiza waliohudhuria mkutano huo.

Naye Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Singida, Adili Elinipenda, alisema taasisi hiyo imeokoa Sh. milioni 33.5 katika kipindi cha Julai hadi Oktoba, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Elinipenda, taasisi hiyo pia imetoa mafunzo mafupi ambayo yatahusisha watumishi wanaotegemea kustaafu na ambao wameshastaafu, wakopeshaji na benki.

Mafunzo hayo, alisema yalilenga kuwafundisha wastaafu juu ya namna bora ya kukopa fedha badala ya kwenda kupata maumivu kwenye taasisi ambazo hazijasalisha.

# Bil. 5.4/- zatumika kuimarisha kilimo

**Na Romana Mallya**

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limetumia Sh. bilioni 5.4 kununua matrekta 26 na zana zake za kilimo ambazo zimeongeza ulimaji kutoka ekari 8,517 msimu uliopita hadi ekari 12,345 kwa sasa.

Mkuu wa Jeshi hilo, Meja Jenerali Charles Mbuge, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akipokea matrekta tisa na zana za kilimo zilizogharimu Sh. bilioni 1.33 ikiwa ni mwendelezo wa ununuzi wa vifaa hivyo.

Jenerali Mbuge alisema msimu wa mwaka 2019/20 walianzisha mpango wa kilimo cha dharura kwa kulima hekari 2,200 zikiwamo ekari 1,000 za mahindi, ekari 200 za maharagwe huko Rukwa na ekari nyingine 1,000 za mpunga eneo la Chita mkoani Morogoro.

Alisema vikosi vingine vililima jumla ya ekari 6317 na kusababisha JKT kuwa na jumla ya ekari 8,517 katika msimu huo uliopita.

"Kwa sasa tuko katika maandalizi ya msimu wa kilimo kwa mwaka 2020/21 katika mashamba maalum ya kilimo cha mkakati. Jumla ya ekari 6,600 zikiwamo ekari 1300 za mahindi (Rukwa), ekari 1,000 za mahindi (Ruvuma), ekari 1,200 za mahindi (Tanga), 600 za maharagwe (Arusha), ekari 2500 za mpunga (Morogoro)." alisema. Pia alisema vikosi vingine navyo vinatarajia kulima hekari 5745 za mazao mbalimbali na kufanya katika msimu huu kuwa na hekari 12,345.

Pia alisema jeshi hilo limeanzisha ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji mkoani Morogoro ambapo utakapokamilika utawezesha utekelezaji wa kilimo cha uhakika na kuleta tija kwa taifa.

Jenerali Mbuge alisema wamenunua matrekta tisa na mengine matano yakiwa na zana zake za kilimo yaliyogharimu Sh. bilioni 1.33 kwa fedha za ndani ambayo yamepokelewa jana. "Kipindi cha takribani mwaka mmoja tangu nimeteuliwa nimezindua matrekta 26, magari 27, mitambo saba, pikipiki 12, vyote vikiwa na thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 5.4 zinazotokana na vyanzo vya ndani," alisema.

Alisema utekelezaji wa kilimo cha mkakati maeneo mbalimbali nchini ikiwamo morogoro ambako kunajengwa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji kitawezesha kutoa elimu kwa wananchi na kupata mbegu bora. Aliwataka watendaji wa jeshi hilo kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii ili kutekeleza matakwa ya serikali ya awamu ya tano na kuwa na chakula cha kutosha.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Kaimu Mkuu wa Utawala JKT, Kanali Hassan Mabena, alisema matrekta hayo na zana nyingine zataelekezwa katika vikosi vya jeshi hilo ili kuhakikisha wanalima kwa uhakika zaidi.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya SumaJKT, Meja Jenerali Farah Mohamed, alisema uwezo wa jeshi hilo kujikwamua katika kilimo wanao kwa sasa hivyo ametaka wajielekeze namna ambavyo heka moja itakavyoweza kutoa mazao mbalimbali.

# Wamiliki shule zisizosajiliwa kukiona

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imewaonya watu wanaoanzisha shule bila kuzisajili na kusababisha taharuki kwa wanafunzi na wazazi unapofika wakati wa mitihani.

Onyo hilo lilitolewa jana na Ofisa Elimu Mkoa wa Dar es Salaam, Abdul Maulid, wakati wa mahafali ya 21 ya Shule ya Sekondari ya Mbezi Beach, jijijini Dar es Salaam. Katika mahafali hayo, wanafunzi 208 wa kidato cha nne wanatarajiwa kufanya mitihani mwezi ujao.

Alisema kumezuka tabia ya baadhi ya watu kukusanya wanafunzi na kujifanya kuwa ni shule, hivyo kuwakosesha wanafunzi hao kufanya mitihani kwa kuwa shule hizo zinakuwa hazijasajiliwa.

Maulid alisema milango ya serikali iko wazi muda wote kwa wale wanaotaka kusajili shule, hivyo hakuna sababu yoyote ya kuanzisha shule bubu na kuwasababishia matatizo wanafunzi na walezi wakati wa mitihani.

Ofisa elimu huyo aliipongeza shule hiyo kwamba ni moja ya zile ambazo zimekuwa zikifanya vizuri sana kwenye mitihani ya kitaifa na aliwataka wasibweteke na badala yake waendeee kufanya vizuri.

"Mbezi Beach ni shule ambayo imekuwa ikifanya vizuri sana kwenye mitihani ya kitaifa na kwa kweli mnatoa mchango mkubwa sana kwa serikali kuboresha elimu nchini, hapa daraja la nne wala 0 si historia ya shule hii. Tunatarajia daraja la kwanza na la pili tu," alisema Maulid.

"Nimetembelea kwenye maonyesho ya kitaaluma nimeona madaktari na wahandisi watarajiwa pale kutokana na umahiri waliouonyesha wakati wakielezea yale waliyoandaa kwa wazazi, naupongeza uongozi wenu na walimu," alisema.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Kiramuu Mbowe, aliishukuru serikali kwa namna ambavyo imekuwa ikiijali shule hiyo hasa wakati wa ugonjwa wa Corona ambapo iliwaletea mapima kwaajili ya kunawia.

Aliwashukuru pia wazazi na walezi wa wanafunzi kwa namna walivyoshirikiana na shule katika malezo jambo ambalo limewarahishia shughuli ya ufundishaji kutokana na wanafunzi kuwa na nidhamu.

Mbowe alisema shule hiyo iko vizuri kitaaluma kutokana na kuwa na walimu mahiri na kwamba anaamini kwa namna walivyopikwa, wanafunzi wote wa kidato cha nne watafaulu kwenye mitihani yao ya hivi karibuni kwa alama za juu.

"Wazazi mmetembelea maonyesho ya kitaaluma asubuhi mliona uwezo mkubwa wa wanafunzi namimi sina wasiwasi kwamba wote hawa watafanya vizuri. Shule hii huwa haitoi daraja 0 hata siku moja" alisema Mbowe.

Mbowe alimuomba mgeni rasmi kuwapatia vitabu na vifaa vya maabara shule binafsi kama ambavyo wanafanya kwa shule za umma kwani zote zinasomesha wanafunzi wa Watanzania.

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu, Hamidu Awadhi, alisema mazingira mazuri ya kusomea na walimu mahiri ndiyo sababu ya kufanya vizuri kwenye mitihani ya ndani na nje ya shule hiyo.

Awadhi Alisema hata kwenye mitihani yao ya kidato cha pili asilimia 90 ya wanafunzi hao walipata ufaulu mzuri kutokana na maandalizi mazuri yaliyofanywa na walimu kwa kushirikiana na uongozi wa shule hiyo.



Mkuu wa shule ya sekondari ya Mbezi Beach, Kiramuu Mbowe akizungumza kwenye mahafali ya 21 ya shule hiyo, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Ofisa Elimu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abdul Maulid na Makamu Mkuu wa shule hiyo, Enosh Sijale na mwalikwa Juma Omar. Kushoto kabisa ni mkuu wa taluma wa shule hiyo, Amiri Joho. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# CRB kuendesha mikutano kikanda kuwainua makandarasi wazalendo

**Na Joseph Mwendapole**

BODI ya Usajili wa Makandarasi (CRB), imepanga kufanya mwendelezo wa mikutano ya kanda na makandarasi wazalendo ikiwa ni mkakati wa kuwajengea uwezo ili waongeze ufanisi katika kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Msajili wa Bodi hiyo, Rhoben Nkori, wakati akifunga mafunzo ya siku moja kwa makandarasi hao.

Mafunzo hayo yalihusu namna makandarasi wazalendo wanavyoweza kuungana na kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi wa miundombinu na namna bora ya kulipa kodi za serikali zikiwamo zile za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

"Bodi inaona umuhimu wa kwenda tena kwenye kanda zetu na kufanya mikutano ya mwaka ambayo ni minne itakayofanyika Mwanza, Mbeya, Arusha na Dar es Salaam na itaanzia Machi mwakani na itaishia Mei. Mkutano wa mwisho wa kilele utafanyika Dar es Salaam," alisema Nkori.

Alisema makandarasi wengi wa Tanzania ni wadogo wakati makandarasi wa nje ni wachache lakini wanatekeleza miradi mikubwa, hivyo wanawapa mafunzo ya kuungana ili wafanye miradi mikubwa ya ujenzi wa miundombinu.

"Makandarasi wana uwezo tofauti wapo wenye uwezo wa kifedha wenye uwezo wa kimitambo na wako ambao ni wataalamu zaidi kwenye fani hivyo wakiunganisha nguvu zao wanaweza kufanya miradi mikubwa kwa wakati na kwa viwango bora zaidi," alisema.

Mkandarasi Christopher Nyagaswa ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Ostrich, alisifu mkakati wa bodi hiyo kuwajengea uwezo makandarasi wazalendo kupitia mafunzo hayo ili waweze kushindana na wenzao wa nje.

Alisema mafunzo hayo yamekuwa yakiwasaidia makandarasi kuongeza ufahamu kuhusu mambo mbalimbali ya namna bora ya kulipa kodi kwa mamlaka ya mapato na umuhimu wa kuungana.

"Mkandarasi mzoefu ambaye ameshiriki kwenye kazi za ubia kwa muda mrefu ametupa uzoefu wa namna ya kuungana, changamoto zake na tahadhari kuingia kwenye ubia ambao unaweza usiwe na manufaa tunaomba muda wa mafunzo," alisema Nyagaswa aliiomba CRB kuendelea kutoa mafunzo ya aina hiyo kwenye kanda zote nchini ili kuwafikia makandarasi wengi wazalendo na kuwajengea uwezo wa kushindana kwenye zabuni kubwa.

Nyagaswa alisema makandarasi wazalendo wanakabiliwa na changamoto ya mitaji ikiwamo masharti magumu ya ukopaji kwenye taasisi za fedha kwaajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi.

"Nitoe rai kwa serikali yetu iendelee kutuwekea mazingira mazuri yatakayotuwezesha kujenga uwezo wa kushindana na wenzetu wa nje," alisema.





# Wakulima wataka suluhu na wafugaji

**Na Peter Mkwavila,**
KONGWA

WAKULIMA wa Kijiji cha Leganga, Kongwa Mkoani Dodoma, wameiomba serikali kutatua mgogoro uliopo baina yao na wafugaji wa jamii ya kimasai uliodumu kwa muda mrefu.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya wenzake, Mashaka Chiloa alidai kuwa jamii hiyo ya wamasai wamekuwa wakikata miche ya mikorosho waliyopanda jambo ambalo linawarudisha nyuma kimaendeleo.

Chiloa alisema kuwa wanalazimika kuiomba serikali ili watatuliwe suala hilo ambalo limechukua muda mrefu.

Alisema kuwa wafugaji hao wamekuwa wakikata miche hiyo iliyooteshwa au kulisha mifugo kwenye mashamba, kitendo ambacho kinahatarisha amani na utulivu. "Hivyo tunaiomba serikali yetu kututatulia suala hili ambalo linaweza kuondoa amani na utulivu kutokana na vurugu tunazofanyiwa na wafugaji hawa kwa kuwa hata usalama wa wakazi wa kijiji hiki ni mdogo, hivyo tunahitaji kuishi kwa usalama na si vinginevyo," alisema.

Mkulima Jackson Makochi, alisema inasikitisha kuona viongozi wanaendelea kuwa kimya pamoja na kupewa taarifa za suala hilo. "Wakulima tunaweza kufikia mahali tukachoka kutokana na tabia hiyo tunayofanyiwa na jamii hiyo ya wafugaji ya kukata mimea yatu mashambani. Sisi tunataka amani na utulivu ndiyo maana tunaiomba serikali kutatua suala hili ambalo hivi sasa linazidi kuwa baya," alisema.

Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji hicho, Anderson Chilingo, alikiri kuwapo kwa mgogoro huo kwa muda mrefu na kwamba unatokanana na baadhi ya wafungaji wa kimasai kulisha mifugo kwenye mashamba ya wakulima na kufyeka miche ya mikorosho.

Chilingo alisema hivi karibuni mkulima mmoja wa kijiji hicho, Mashaka Chiloa, alifanyiwa vurugu kwenye shamba lake la hekari tatu la miche ya mikorosho.

"Ninakiri kuwapo kwa tukio hilo ambalo linafanywa na wafugaji wa kimasai, ambao hivi karibuni walikata miche ya mikorosho ya mkulima mmoja na kusababishia hasara ya mamilioni ya fedha, hivyo ninaiomba serikali yetu sikivu kuingilia kati suala hili ili kuepusha uvunjifu wa amani," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema hofu iliyojengeka kati ya pande hizo, inahatarisha maisha ya wakazi hao.



Mkulima wa Kijiji cha Leganga, wilayani Kongwa, mkoani Dodoma, Jackosn Makochi (80), akizungumza na waandishi wa habari kijijini hapo juzi, akilalamikia wafugaji wa jamii ya Kimaasai kuchunga mifugo kwenye mashamba yao. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Jiji lahimiza uchunguzi afya mifugo

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imewataka wakazi wa jiji hilo kujenga tabia ya kuifanyia uchunguzi wa magonjwa mifugo yao katika maabara ya mifugo Kanda ya Kati.

Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri hiyo, Gratian Mwesiga, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kati ya wataalam wa mifugo na Wakala wa Maabara ya Veterinari.

"Uwapo wa maabara hii ni jambo la manufaa katika utendaji kazi, kwa kuwa tupo katika jiji ambalo ni makao makuu, hivyo hatutakiwi kufanya kazi kwa kubahatisha," alisema Mwesiga.

Alisema utekelezaji wa majukumu yao lazima uendane na hadhi ya makao mkuu ya nchi na kuwataka wananchi kujenga utamaduni wa kuchunguza mifugo yao kwa kuwa wataalam wapo kwa ajili hiyo.

Alisema, kuwa katika uchunguzi wa magonjwa, wataalam hawatakuwa wakitibu mifugo kwa kubahatisha na magonjwa yote yatakuwa yanachunguzwa kabla hayajaanza kutibiwa.

"Tulizoea kutibu kwa kutazama dalili za ugonjwa kwa sababu hatukuwa na namna ya kuchunguza," alisema Mwesiga.

Alitoa wito kwa wafugaji kutokubali mifugo yao kutibiwa bila kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara na kubaini tatizo.

Alisema ugonjwa unaotibiwa lazima uchunguzwe kwanza na kufahamika, ndiyo matibabu yaanze na kuwataka maofisa mifugo katika ngazi ya mitaa, kata na halmashauri kuacha tabia ya kutumia dawa ovyo kwa mifugo.

Aidha, aliwataka wazalishaji wa vyakula vya mifugo na wafugaji kutumia fursa ya maabara hiyo kupima ubora wa vyakula vya mifugo.

"Katika Halmashauri ya Jiji kumekuwa na malalamiko kwamba baadhi ya vyakula vya mifugo vipo chini ya kiwango hili naomba mliangalie,"alisema Mwesiga. Alisema waitumie maabara hiyo kupima ubora wa vyakula hivyo vinavyotumika katika mifugo ili kuwe na mifugo bora na mfugaji asipate hasara.

"Hili ni muhimu, unaweza kukuta mfugaji anajitahidi kutibu magonjwa yote, ila chakula kama ni kibovu, mifugo itaendelea kufa," alisisitiza Mwesiga.

Kwa upande wake, Meneja wa Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) Kanda ya Kati Dodoma, Dk.Japhet Nkangaga, alisema kuwa kikao kazi hicho pamoja na mambo mengine kililenga kubainisha mbinu mbalimbali wananchi.

Alisema wataalamu wa mifugo wajibu wao ni kuangalia na kulinda afya za wanyama ili kudhibiti magonjwa yoyote ambayo yanaweza kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu.

"Wito wangu kwa wananchi, kwanza washirikiane zaidi na wataalamu wa mifugo, wasitibu wala wasihisi kwamba kuona dalili fulani wakaamini kwamba ni ugonjwa fulani, wasiende kwa mazoea,"alisema.

Alisema mnyama akitibiwa bila kufuata utaratibu, binadamu akala nyama bado kunakuwepo na mabaki ya dawa katika mwili wa mnyama.

# DC aonya uharibifu miundombinu ya maji

**Na Augusta Njoji,** BAHI

MKUU wa Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, Mwanahamisi Munkunda, amewataka wakazi wa kijiji cha Msisi kutoruhusu kufanyika uharibifu wowote wa miundombinu ya mradi wa maji wa Mundemu AP ili uwahudumie kwa muda mrefu.

Akizungumza juzi na wananchi hao baada ya kukagua mradi huo, mkuu huyo alisema ili kurahisisha utunzaji wa mradi huo ni vyema kikaundwa chombo maalum cha watumiaji maji kitakachokuwa na jukumu la kusimamia utunzwaji wa miundombinu na matumizi ya fedha.

"Pamoja na kuwa tuna mradi huu mzuri bila kuutunza ni kazi bure, najua wagori ng'ombe wanatabia ya kudharau sana,na hapa nasikia sikia kengele ya ng'ombe na baada ya muda utaona mtu ameshaingiza mifugo, hiyo haikubaliki,"alisema.

Alisema mitambo ya umwagiliaji iliyopo kwenye mradi huo haitaki kukanyagwa hata na mbuzi hivyo wahakikishe hakuna mifugo itakayoingia.


"Hapa chagueni mwenyekiti wa kusimamia huu mradi, maana tukimtumia mwenyekiti wa kijiji tutakwamisha utendaji kazi kutokana na majukumu mengi aliyonayo, chagueni mwenyekiti miongoni mwenu ili akizembea tuweze kumwajibisha,"aliongeza Mkuu huyo.

Mratibu wa Mradi wa Mundemu AP, Zacharia Shigukulu, alisema mradi huo ulianza rasmi mwaka 2017 mwishoni kwa kufanya utafiti wa maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, kilimo na mifugo.

Alitaja lengo la mradi huo kuwa ni kuwanufaisha wakazi wa vitongoji vya Majengo A, Majengo B na Chambuli vyenye jumla ya kaya 406 na wakazi wapatao 1,665 na mifugo zaidi ya 2,700.

Mratibu huyo alisema hadi kufikia mwaka jana mradi ulikuwa umetumia zaidi ya Sh.Milioni 97 ambapo kwa sasa Shirika la World Vision limeendelea kutafuta fedha zaidi ili kukamilisha malengo yake.

Alisema kutokana na juhudi hizo wamefanikiwa kupata fedha kwa ajili ya miradi miwili tofauti ambayo ni mradi wa umwagiliaji utakaogharimu Sh. milioni 47 na pia kupata fedha kwa ajili ya mradi wa kusambaza maji utakaogha-





## Ukosefu fedha watajwa sababu za kushindwa

**Na Rahma Suleiman,**

ZANZIBAR

UKOSEFU wa fedha za kuendesha kampeni kwa vyama vya upinzani pia ni chimbuko la kufanya vibaya katika uchaguzi wa mwaka huu.

Hayo yalielezwa na baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani, akiwamo Mjumbe wa Baraza Kuu la Chama cha Wananchi (CUF), Nassor Seif Amour, alipokuwa akizungumzia anguko la wapinzani katika uchaguzi wa mwaka huu.

Alisema vyama vya upinzani vimeingia katika uchaguzi vikiwa vinakabiliwa na hali ngumu ya fedha jambo ambalo limeathiri kampeni na kushindwa kuwafikia wapigakura.

"Ukosefu wa fedha ulikuwa tatizo kubwa. Tumeshindwa kuwafikia wapigakura wengi lakini upinzani unaelekea kubaya kwa matokeo haya," alisema.

Alisema mtazamo wa kisayansi unaonekana kuna mbinu zimetumika kuhakikisha wapinzani wanapoteza idadi kubwa ya majimbo licha ya kuwa na wafuasi wengi Zanzibar na Tanzania Bara.

Mwanasiasa huyo alisema mgombea urais wa CCM, Dk. Hussein Mwinyi, kampeni zake zilikuwa za kisayansi ikiwamo kutumia vyombo vya habari kurusha matangazo yake moja kwa moja pamoja na ziara zake maalum za kuyafikia makundi maalum na kusikiliza kero zao.

"Ameyafikia makundi mengi katika jamii, kampeni zake zilikua za kisayansi tofauti na sisi wapinzani. Tumeshindwa hata kufanya mikutano mingi ya kampeni kwa mujibu wa ratiba ya tume ya uchaguzi," alisema.

# CUF yamtaja Maalim Seif uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha Wananchi (CUF) kimesema mgogoro wa uongozi uliojitokeza na kusababisha aliyekuwa katibu mkuu, Maalim Seif Sharif Hamad, kufukuzwa, umesababisha kupoteza viti vyote vya uwakilishi na ubunge Zanzibar.

Mjumbe wa Baraza Kuu na mwasisi wa chama hicho, Nassor Seif Amour, alisema hayo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu matokeo na matukio yaliyojitokeza kabla na baada ya uchaguzi mkuu.

Alisema mgawanyiko wa viongozi umewagawa mpaka wanachama baada ya kundi moja kujitenga na kumesababisha baadhi ya wananchi kubaki CUF na wengine kumfuata Maalim Seif baada ya kujiunga na ACT Wazalendo.

Amour alisema tokea kuanzishwa kwa CUF, ngome yake ya kisiasa imekuwa kisiwani Pemba na kudhibiti majimbo 18 kisiwani humo, lakini uchaguzi wa mwaka huu, matokeo yamekuwa mabaya na kulazimika kupata kiti kimoja kati ya majimbo 18. Mwelekeo wa vyama vya upinzani, alisema ni mbaya lakini sehemu kubwa umesababishwa na viongozi wa vyama vya siasa kwa kuweka mbele maslahi binafsi badala ya matumaini ya wanachama waliyoyaonyesha tokea mfumo wa vyama vingi mwaka 1992. "Wananchi walionyesha matumaini makubwa na vyama vya upinzani bahati mbaya viongozi baada ya kuchaguliwa wameshindwa kuthamini," alisema.

Alisema pamoja na kasoro zilizojitokeza katika uchaguzi wa mwaka huu, sehemu kubwa ya matatizo yametokana na waliokuwa viongozi wa CUF kususia uchaguzi wa marudio wa mwaka 2016 na kusababisha CCM kupata nafasi ya kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali ya uchaguzi na kanuni zake ikiwemo kura ya mapema.

Alieleza mabadiliko ya sheria hiyo, yameathiri mfumo mzima wa demokrasia katika upatikanaji wa viongozi na wa kulaumiwa ni waliokuwa viongozi wa CUF wakiongozwa na Maalim Seif na wezake waliojiunga ACT Wazalendo.

"Chama cha Mapinduzi kimenyakua majimbo mengi kisiwani Pemba pamoja na viti vyote 32 Unguja likiwemo jimbo la kihistoria la Malindi ambalo limekuwa likichukuliwa na wapinzani tokea kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi," alisema.

Wakati chama cha CUF ikiambulia kiti kimoja Kisiwani Pemba Jimbo la Mtambile, Chama cha ACT Wazalendo kimeambulia viti vinne vya uwakilishi licha ya wanachama wengi wa CUF kujiunga na chama hicho.



Rais Mteule wa Zanzibar kupitia CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akiwasalimia wananchi baada ya kutangazwa mshindi na Tume ya Uchaguzi Zanzibar juzi usiku. **PICHA: ANTHONY SIAM**

# Rais mteule Mwinyi apewa ushauri

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS Mteule Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameshauriwa kuunda serikali itakayokuwa na uwezo wa kusimamia uwajibikaji wa utumishi wa umma pamoja na kupambana na rushwa.

Sambamba na hayo, ameshauriwa kuunda serikali itakayopambana na ufisadi na kuondoa migogoro ya ardhi Zanzibar.

Baadhi ya wananchi walitoa maoni hayo walipokuwa wakizungumzia kukamilika kwa uchaguzi mkuu na mwelekeo wa Zanzibar katika kuimarisha misingi ya utawala bora na uchumi.

Mbunge wa zamani wa Kikwajuni, Parmuk Singh Hoogan, alisema serikali ya awamu ya nane inatakiwa kuongozwa na watu wanaochukia rushwa, ufisadi na kuwa na uwezo wa kupambana na migogoro ya ardhi ambayo imekuwa kero kwa wananchi wa Zanzibar.

"Kwanza nampongeza Dk. Mwinyi kwa ushindi lakini serikali ya awamu ya nane wanatakiwa viongozi wake wawe watu wanaochukia kukosekana uwajibikaji kwa watumishi wa umma, rushwa, ufisadi na wawe karibu na wananchi," alisema.

Hoogan alisema Dk. Mwinyi ni mtu muungwana na ameonyesha nia ya kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar kuondoa ukabila, udini, utabaka kutokana na ahadi zake alizokuwa akizitoa wakati wa kampeni na sasa wakati wa utekelezaji umefika.

Hamad Mamoja Ngwali, mfanyabiashara eneo la Darajani, alisema wanatarajia kuona serikali inaimarisha sekta muhimu za kiuchumi na kuleta mabadiliko katika sekta ya biashara Zanzibar.

Alisema wafanyabiashara wadogo wanahitaji kuona mazingira ya biashara yanakuwa mazuri badala ya kuimarishwa ulinzi na kuwafanya washindwe kufungua maduka yao.

"Uchaguzi umemalizika tunahitaji utulivu tuendelee na biashara zetu ndiyo maana unaona tumefunga maduka na tuko nje baada ya kuambiwa tusifungue kutokana na hofu ya uchaguzi," alisema Ngwali.

Pia Rais huyo mteule ameshauriwa kuunda tume maalum ya kushughulikia migogoro ya ardhi Zanzibar kwa sababu kuna wananchi wengi wanyonge wamenyang'anywa ardhi na baadhi ya viongozi na watendaji wamehusika katika hilo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
UDANI
TELE

JUMAMOSI OKTOBA 31, 2020



MASHALLAH..NICKI UMEKUWA MAMA Uk.14





# WAWILI WAMEINGIA

## Wawili wametoka

WASANII wawili watakuwa miongoni mwa wabunge wapya waliofanikiwa kupita katika upigaji kura uliofanyika Oktoba 28 mwaka huu.

Wabunge hao wateule, Shabani Taletale, jina la usanii anaitwa 'Babu Tale' (jimbo la Morogoro Kusini) na Hamisi Mwinjuma, maarufu kama Mwana FA (Muheza), wataingia mjengoni kwa mara ya kwanza kula kiapo ili kuanza kazi rasmi ya kuwatumikia wananchi wao.

Hata hivyo, imekuwa vilio wanamuziki, Joseph Mbilinyi anayejulikana kama 'Sugu' (Mbeya Mjini) na aliyekuwa mbunge wa Mikumi, Joseph Haule, maarufu kama 'Profesa Jay', ambao wote wawili wameangukia pua katika uchaguzi huo.

Pamoja na kuwakilisha vyema bungeni katika vipindi tofauti, safari hii wataendelea kutazama vikao vya bunge wakiwa majumbani mwao, huku wakisuka mikakati ya kurudi tena jukwaani.

Babu tale na Mwana FA, ni wanamuziki wakongwe katika muziki wa Bongo Fleva, hivyo kuingia kwao bungeni kutasaidia kupeleka vilio vya wasanii nchini ambao licha ya kufanya kazi kubwa, lakini wanaishia kuwa masikini.

Wabunge hao wateuli wahakikishe wakiingia katika chombo hicho cha kutunga sheria, wayafanyie kazi yale ambayo wenzao walishindwa ili kuwapatia neema wasanii wa fani zote.

BASI SAWA

## Faiza amtuliza Sugu kupoteza jimbo



MWIGIZAJI na mjasiriamali, Faiza Ally, amemtuliza mpenzi wake wa zamani na baba wa mtoto wake, Joseph Mbilinyi, maarufu kama 'Sugu' baada ya kushindwa nafasi ya Ubunge Jimbo la Mbeya Mjini.

Sugu alitupwa nje na Dk. Tulia Ackson wa Chama Cha Mapinduzi baada ya kushinda kiti hicho kwa kumzisi kura zaidi ya 8000.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram Faiza Ally, ameandika "Tulikupendaga, tuliendelea kukupenda, tunakupenda zaidi na tutakupenda kila siku , machoni mwetu na kwenye mioyo yetu wewe ni mshindi toka mtoto mpaka utazeeka na mpaka siku ya mwisho itakua hivyo hakuna kitakacho badilika, mimi na familia tunakutumia salamu za upendo tunatamani kuwepo ulipo tusheherekee maisha pamoja kwa sababu wewe ni mshindi kwetu, najivunia wewe baba Sasha"

## Mzee Yusuph awa ustadhi wa Ben Pol

MKONGWE wa muziki wa Taarab nchini, Mzee Yussuf, ameahidi kujitolea kumfundisha elimu ya dini ya Kiislam, msanii mwenzake Ben Pol, ambaye wiki iliyopita alitangaza alibadili dini.

Akizungumza kupitia EATV, Mzee Yussuf, amempongeza Ben Pol kwa uamuzi wa kuridhia kuhamia kwenye uislam, hivyo yeye atawajibika kumfundisha Quran.



"Kuingia au kutoka kwenye dini ni fikra, falsafa, utashi na uhiari wake, kama uingiaji wake kwenye Uislam haihusiani na vishawishi, mapenzi au kulazimishwa hatopata tabu kabisa ila kama uamuzi wake utahusiana na hivyo vitu itampa tabu kidogo kwenye nafsi yake" amesema Mzee Yussuf.

Akaongeza "Namshauri ajitahidi kupambana, ajielewe, afahamu na asione tabu, pia nipo tayari kuwa karibu naye kwa ajili ya mambo fulani kama fikra, mawazo na elimu, kama nikipata namba yake basi nawapa wiki 2 ataweza kusoma



## Zee Cuty umeyataka mwenyewe

MWANAMUZIKI wa kike, Zee Cuty, amekanusha kuwa anatoka kimapenzi na Uchebe, akisema yeye anamuona kama shemeji yake kutokana na kumuoa dada yake Shilole.

Zee Cuty, ameamua kujitokeza baada ya video fupi kusambaa katika mitandao ya kijamii akionekana akikumbatiana na Uchebe, na kuibua mjadala mkali.

"Mimi na Uchebe tunafahamiana kwenye mazingira ya kazi na alikuwa mume wa dada yangu Shilole ila kuna watu wanadhani nimeingia kwenye kiki na Uchebe, namuheshimu kama mtu ambaye alikuwa na dada yangu, kilichotokea ni salamu tu na nilikuwa nipo kwenye hali ya ujana fulani hivi" amesema

## Namzika Mwanangu; Kisebusebu na kiroho papo

**Na Adam Fungamwango**

BINADAMU ana mambo mengi ambayo wakati mwingine yanashangaza. Mtu anaweza kufanya jambo ambalo unadhani kuwa amedhamiria kutoka kwenye moyo wake, kumbe anafanya kwa sababu fulani. Kwenye moyo wake anajua kabisa kuwa analolifanya si analolitaka.

Hebu leo tuiangalie filamu ya 'Namzika Mwanangu'. Ni filamu yenye mafunzo bora kwa jamii. Imechezwa na wasanii chipukizi tu kama Nyamizi Shaaban aliyecheza kama Nyamizi, Macky Daimu aliyecheza kama Macky, Neema Deus kama Neema na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha watu wawili, mwanamke na mwanamume wanagombana. Mwanamume anamwambia mwanamke kuwa huyo mtoto aliyekuwa naye si wa kwake na amtafute baba yake.

Mwanamke anamwambia mtoto yule ni wake na anachotaka ni matunzo tu ya mtoto wa si vinginevyo. Ambroce, ambaye ndiye mwanamume mwenyewe anamwambia aache kumfuatafuata, mapenzi yao yalishaisha zamani.

Nyamizi jina la mwanamke yule anabaki na kichanga chake. Anamlea kwa shida. Tabu zilipozidi na kazi hana aliamua kuingia kwenye majaribu, baada ya kupata mwanamume mwingine aitwaye Macky kwa ajili tu ya kupata pesa ya maziwa na chakula kwa mtoto wake.

Hata hivyo, alimficha mpenzi wake huyo kama ana mtoto.

Siku za mwizi arobaini, kwani wakati yupo na mpenzi wake Macky walipata vinywaji baridi, ilipigwa simu kuwa mtoto wake anaumwa ghafla. Hiyo ilimfanya kuaga haraka kwa namna iliyomshangaza mpenzi wake. Alipohoji sana ndipo Nyamizi alipofunguka kuwa ana mtoto.

Macky alimwambia hawezi kuwa na mwanamke wa aina hiyo na akampa sharti ili amuoe ni lazima huyo mtoto ama ampeleke kwa baba yake, au amuue.

Macky anampa kazi rafiki yake kumfuatilia Nyamizi, kwani amempa mtihani mkubwa na ambao huenda akaufanya.


Na kweli, mwishowe, Nyamizi anaamua kwenda kuchimba shimo na kumzika mtoto wake mzima mzima, ili mradi tu awe na Macky, kutokana na mazingira magumu anayoishi, huku baba wa mtoto akiwa hana msaada wowote.

Macky na rafiki yake wanafanikiwa kumkuta hajakamilisha azma hiyo, lakini tayari akiwa amechimba shimo.

Kitendo kile kilimtisha Macky na kusema kuwa hawezi kuwa na mwanamke kama yeye kwa sababu ni katili.

Nyamizi anachanganyikiwa. Sasa amekataliwa na mzazi mwenzake, lakini pia mpenzi wake mpya aliyekuwa anamtegemea Macky naye amemgeuka.






## Mhh! Gigy Money hukosagi vituko

Msanii mwenye tabia za utata, Gigy Money, amewachambua mashabiki wake wanaotumia mtandao wa Instagram, akisema ni watu wanaoleta msongo wa mawazo.

Gigy Money, amewataja watu hao wana sifa, wapo wale wanaotumia Instagram 'kulike' picha au video kutumia akaunti zao feki, ila 'komenti' zao utatami kufunga ukurasa haraka, na kuna wale wanajiona wapo daraja la juu ambao wanajifanya kurasa zao biashara"

Akamalizia kwa kusema "Halafu kuna hawa ambao kama hawapo wao nikutumiana 'DM' nakusave matukio, sasa huko DM mnatunyambua kama nyinyi mnaweza kuvumilia, pia hawa wakutumiana DM ni wambea sana."






## Bendi za Maafande jeshini

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI wa utawala wa Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kila Shirika na Kampuni nchini lilikuwa ama lina timu na mpira wa miguu, netiboli, mpira wa kikapu, ngumi, bendi za muziki wa dansi, taarabu au vyote kwa pamoja.

Na bendi za muziki wa dansi hazikuwa kwenye mashirika na kampuni peke yake, bali hata kwenye majeshi yetu ya ulinzi na usalama.

Leo tutaziangazia bendi za majeshi ya Tanzania. Lengo lilikuwa ni kuwaburudisha makamanda wapiganaji kila wikiendi, wakati mwingine na familia zao.

Kiufupi hazikuwa bendi za mchezo mchezo, kwani zilikuwa maarufu na tishio kwa bendi za raia, ziwe za kampuni, Mashirika au za watu binafsi.

**MWENGE JAZZ BAND**

Hii ndiyo unaweza kusema kama bendi mama ya zote iliyomilikuwa na jeshi. Wenyewe walipenda kuiita 'Mwenge ya Mashujaa'.

Ilikuwa ni bendi tishio na maarufu zaidi ya bendi zote, ikikusanya wanamuziki mahiri nchini Tanzania. Ilikusanya vijana wa Kitanzania wenye vipaji na kuwapa ajira za muziki, na jeshi pia.

Hata hivyo kuna wengine walibakiwa kuwa wanamuziki tu. Bendi hii ipo mpaka sasa, ingawa haina nguvu zile kama za mwanzo ilipokuwa ikishindana na bendi kubwa kama za Msondo na Sikinde.

Inamilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ). Ilivuma sana katikati ya miaka ya 1970 hadi katikati ya miaka ya 1980.

Kwa nyakati tofauti ilikuwa na wanamuziki nyota kama Benovilla Antony, Mgolo Mohamed, Mohamed Salum 'Gotagota', Msafiri Haroub', Luza Elius na wengine wengi.

**POLISI JAZZ BAND**

Ilikuwa ni bendi ya pili kwa ukubwa na umaarufu kwa bendi za majeshi, ukiondoa Mwenge Jazz Band.

Hii inamilikiwa na Jeshi la Polisi la Tanzania, Makao Makuu yake yakiwa maeneo ya Kilwa Road, maeneo ya Kurasini jijini Dar es Salaam.

Iliwika sana miaka ya 1978, hadi 1981 wakati ilipokuwa na wanamuziki mahiri kama Tx Moshi William, Kassim Mapili, Jalala Ally na wengineo. Ilipendwa mno na mashabiki wa muziki wa dansi Tanzania kwa vibao vyao kama 'Tuli', 'Mwaka wa Watoto', 'Mayasa', 'Wivu Sina' na nyingine nyingi. Bado ipo, ingawa imepungua makali yake.

**MAGEREZA JAZZ BAND**

Ni bendi inayomilikuwa na Jeshi la Magereza. Haikuwa maarufu sana kuliko zingine. Lakini kuna wakati ilikuwa ikitoa nyimbo chache zilizopendwa.

Hata hivyo, bendi hii ilijinyakulia umaarufu wa muda mfupi, ilipowachukua wanamuziki kama Abel Bathazar, Hassan Kunyata, Nana Njige na wengineo mwanzoni mwa miaka ya 1990 na mtindo wao wa 'Mkote Ngoma, Kubali Yaishe' na kutoa vibao vilivyoondokea kuwa gumzo kama 'Edina', 'Ashura' na nyingine nyingi.

**JKT KIMBUNGA STEREO**

Bendi hii ilikuwa ya kawaida, lakini ilipomchukua John Simon kutoka Nuta Jazz, ndipo ilipoanza kupiga muziki wa ushindani.

Iliwaleta baadhi ya wanamuziki kama Mwarami Said ambaye baadaye alikwenda Sikinde, na kutoa vibao kama 'Cheza Rhumba Kimbunga', 'Ushirikina', 'Chakula Cha Shida' na nyinginezo.

Bendi hii ilimilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

**JKT MAFINGA 'KIMULIMULI'**

Pia bendi hii ilimilikiwa na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), lakini haikuwa Dar es Salaam, bali mkoani Iringa. Ilikuwa ni kama kikosi cha pili cha JKT Kibunga. Ni kwamba baadhi ya wanamuziki walioonekana wamekosa nafasi Kimbunga walipelekwa Iringa. Walimpata pia Zahir Ally Zorro wakafanya kazi ya maana.

Wimbo wao wa kwanza ambao uliwafanya kuanza kuwa maarufu na bendi tishio si kwa JKT Kibunga yenyewe tu, bali hata bendi nyingine ni 'Christina' uliotoka mwaka 1977, uliotungwa na kuimbwa na Zahir.



# Kim Karashian kivyakevyake

MWANAMITINDO na mshiriki wa kipindi cha maisha halisi kwenye Televisheni, Kim Kardashian, katika hali isiyo ya kawaida amesherehea miaka 40 ya kuzaliwa kwake akiwa na ndugu na rafiki zake wa karibu.

Katika hafla iliyoandaliwa na Kardashian, hakuwepo mme ake Kanye West, jambo ambalo linaashiria wawili hao wapo katika mgogoro ndani ya ndoa yao.

Katika posti aliyoiweka katika akaunti yake ya Istagram, mrembo huyo aliwashukuru ndugu na rafiki zake kwa kuwa karibu naye katika muda huo.



## Pole Ada, yote muachie Mungu

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nolywood, , ameomba mashabiki wake kumuombea wakati anakwenda kumzika mtoto wake wa pekee.

Katika video fupi ambayo ameiweka katika ukurasa wake wa Istagram, Ada amesema dua pekee ndiyo itakayomsaidia wakati huu mgumu anaokabiliana nao.

Mazishi ya mtoto wake huyo yanafanyika nje ya mji wa Lagos, ambapo Ada amesafiri kwa ndege maalum akiwa na ndugu zake wa karibu.


## Mashallah.. Nicki umekuwa mama

RAPA maarufu wa kike kutoka Marekani, Nicki Minaj, kwa mara ya kwanza ametoa picha ya mtoto wake wa kiume.

Nicki, amepiga picha hiyo wakati akisherehekea mwaka mmoja wa ndoa yake na mumewe Kenneth Petty.

Mtoto huyo ambaye alizaliwa wiki kadhaa zilizopita, alipokelewa vizuri na mastaa mbalimbali wakiwamo wasanii wenzake wa muziki na waigizaji wa Holywood.





## Nengi wasiwasi ni akili ujue!

MSHIRIKI wa shindano la Big Brother Nigeria (BBNaija), Nengi,hapendi uhusiano na mtu ambaye hana mapenzi ya dhati.

Akizungumza kupitia kupitia mtandao wa Istagram live, Nengi amesema mpenzi wake ameanza kushindwa kutokana na kumpa ahadi hewa.

Wawili hao wapo kwenye mahaba mazito na waliamua kuwashirikisha mashabiki zao kuelezea hisia zao.

## Craze Clown mshukuru Mungu

MSANII wa vichekesho wa Nigeria, Emmanuel Ogonna Iwueke, ambaye anafahamika kama Craze Clown, amenusurika katika ajali mbaya ya gari.

Katika ujumbe wake aliouweka kwenye ukurasa wake wa Istagram, aliandika kwamba amenusurika kifo baada ya gari alilokuwa akisafiria la aina ya BMW kupata ajali mbaya.

"Mungu umenusuru maisha yangu wakati wa siku ya kuzaliwa mke wangu, nitasimulia baadae , lakini kwa sasa nashukuru kwa kusaidia maisha yangu," ameandika.



MAKALA

Na Mwandishi Wetu

MAKANDARASI wazalendo kwa muda mrefu wamekuwa wakilalamikia kukosa miradi mikubwa ya ujenzi kulinganisha na kampuni za wageni hali ambayo imesababishwa na mitaji midogo na mitambo.

Lakini ili kupambana na hali hiyo kwa muda mrefu serikali imekuwa ikiwataka waungane ili wapate uwezo wa kimtaji na kimitambo wa kufanya miradi mikubwa kama wenzao wa mataifa ya nje.

Ni ukweli usiopingika kwamba ingawa makandarasi wazalendo wanauwezo mkubwa lakini wengine wanazidiwa kimitambo na kimtaji na kampuni kubwa za nje ambazo zimekuwa zikishinda zabuni nyingi za ujenzi wa miradi hasa ile mikubwa.

Bodi ya Makandarasi Nchini (CRB) imekuwa ikiendesha mafunzo ya mara kwa mara kwa makandarasi wazalendo kuwajengea uwezo wa kiteknolojia, kibiashara na kimtaji ili waweze kushindana na kampuni kubwa ambazo huwa zinakuja na mitambo mikubwa.

Hivi karibuni mkoani Arusha Profesa wa uchumi, Prosper Ngowi, alipokuwa akitoa mada kuhusu ujuzi wa usimamizi wa biashara kwenye mafunzo ya siku tatu yaliyoandaliwa na Bodi ya Makandarasi Nchini (CRB) aliweka wazi kuwa badala ya makandarasi kuwa vile vile miaka yote wanapaswa kubuni vitu vipya vitakavyowavutia wateja wao kuwapa zabuni hivyo kuondoa malalamiko ya kampuni za nje kupendelewa

Alisema kampuni washindani kwenye masuala ya ujenzi zimekuwa zikiingia kwenye soko hilo kila mwaka hivyo iwapo makandarasi wazalendo hawatabadilika na kubuni mambo mapya watatolewa nje.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, akikagua mtambo unaotumika katika ujenzi wa Miondombinu mbalimbali.

# Makandarasi wazalendo wakiungana wataleta mageuzi sekta ya ujenzi

Profesa Ngowi aliwaasa makandarasi wa ndani kufanya kazi kwa weledi kwani hakuna mtu atakayetoa kazi kwa kigezo kwamba kampuni husika ni ya mzalendo bali kinachoangaliwa ni uwezo na uzoefu wa kumudu kukamilisha kazi kwa wakati uliopangwa na kwa ubora uliotakiwa.

"Lazima tuambiane ukweli hapa hakuna mtu atakuja kukupa kazi eti kwasababu wewe ni kampuni ya mzalendo, uzalendo hauwezi kuwa kigezo cha kukupa kazi, mtu atakupa kazi kwa rekodi yako iliyotukuka na si vinginevyo," alisema Proofesa Ngowi

Aliwataka wenye kampuni pia kuweka mipango mikakati ya miaka angalau minne ili kujua kampuni hiyo inataka kufika wapi na hata ikitokea dharura akapata matatizo ya kiafya watu waweze kujua ilipokuwa inaelekea kutokana na mkakati uliowekwa.

Profesa Ngowi alisema masoko ni muhimu kwa uhai na ustawi wa kampuni yoyote hivyo makandarasi wanatakiwa kutenga bajeti nzuri kwaajili ya kujitangaza kwa kutengeneza kalenda za mwaka, flana, kalamu, kofia na kuweka nembo zao na mawasiliano yao.

" Ukienda kwenye mikutano ni fursa ya kujitangaza kwa kugawa mawasiliano yako kwa wenzako nguvu ya networking ni kubwa sana kwenye biashara yoyote duniani na bila kujitangaza unaweza usifike mbali kwasababu hakuna atakayejua upo na unafanya nini," alisema Profesa Ngowi.

Alisema kwa kuwa masoko mengi kwasasa yako kwenye mitandao na makandarasi wanatakiwa kuitumia vyema mitandao ya kijamii kutafuta masoko na kutangaza kampuni zao na shughuli wanazozifanya.

Alisema makandarasi wazawa wamekuwa wakilalamikia uduni wa mitaji ingawa wakiungana wanaweza kupata mitaji mikubwa na kutekelezaji miradi mikubwa na kukuza kampuni zao

Profesa alisema kinachozifanya kampuni za wazalendo kushindwa kuungana ni ubinafsi wa baadhi ya wenye kampuni hizo kwani mwisho wa siku wamekuwa wakiishia mahakamani kwenye migogoro.

"Mkiungana mnaweza kushindana na kampuni kubwa ya nje lakini ninachoona ni ubinafsi wa baadhi yetu kwenye hizi kampuni kwasababu faida inapopatikana badala ya kukutana hotelini kugawana mnashinda mahakamani kila mmoja akidai kuwa yeye anastahili mgawo mkubwa," alisema

Kuhusu usimamizi wa kampuni, Prof Ngowi alisema kuna baadhi ya kampuni kubwa zinataka kujua kama kampuni wanayotaka kuipa zabuni ina uongozi thabiti hivyo kama mhusika hana bodi ya uhakika anaweza kukosa zabuni hiyo.

"Kuna watu wanaweka bodi ya wakurugenzi ya magumashi, yaani unakuta mama, baba, watoto, mjomba ndiyo wamo kwenye bodi sasa ukifanya hivi kuna kazi lazima utazikosa kabisa hasa kampuni za nje ambazo zinataka kuona kila kitu kimenyooka," alisema

"Hata kwenye baadhi ya benki hapa nchini ukitaka mkopo sasa watakuambia mwenyekiti wa bodi asaini sehemu na wewe huna mwenyekiti wa bodi utapataje huo mkopo kwa hiyo lazima tuweke mambo wazi na yanyooke kampuni isiwe 'one man show'," alisema

Alisema kwenye kampuni husika kila kitu kinatakiwa kwenda sawa hata kama mkurugenzi au msaidizi wake mkuu hayupo kuanzia kusaini hundi na kusimamia vifaa vya ujenzi kwenye miradi inayoendelea.

"Nyinyi leo mpo hapa je, mambo huko kwenye kampuni zenu yanaendelea au yamesimama, mtu akitaka hundi mpaka wewe uwepo ndipo isainiwe, je mtu akitaka mbao au nondo kwenye ujenzi unaoendelea asubiri mpaka utoke kwenye mafunzo haya, hapana kama unafaanya hivyo unakosea lazima ukasimishe majukumu," alisema

Aliwataka makandarasi hao kuwajengea uwezo wasaidizi wao kama wanaona kuwa hawawezi kukasimu madaraka yao wanapokuwa nje ya ofisi kwa sababu yoyote ile ili kazi ziendeleee na miradi ambayo walikabidhiwa ikamilishwe kwa wakati na kwa ubora ule ule.

"Inamaana kuna mtu hapa kafunga ofisi kuja kwenye mkutano Arusha? Weka watu makini ambao unauhakika kwa asilimia 100 kwamba mambo yanakwenda, usifunge ofisi hata siku moja hii one man show ndiyo inakwamisha kampuni nyingi kushindwa kufika mbali, mimi ni Mkuu wa chuo nikiondoka mambo yanakwenda kama kawaida," alisema Prof. Ngowi.

Alisema baadhi ya wenye kampuni wanaachia baadhi ya majukumu lakini kwenye masuala ya fedha huwa hawaachi mtu mwenye uwezo wa kusaini fedha zitoke hali ambayo inaweza kusababisha miradi kukwama na kushindwa kutekelezwa kwa mujibu wa mkataba na wateja wao hivyo kuingia kwenye migogoro na wateja.

"Najua ni ngumu sana kumwachia mtu kusaini fedha zitoke kwasababu unaweza kukuta watu wamejilipa malipo mengine ambayo hayakuwa ya lazima. Lakini pamoja na hayo lazima utafute namna ya kuacha mtu wa kufanyakazi hiyo fikiria unakwenda likizo ya siku 28 siku zote hizo kama feedha hazitoki utakwamisha shughuli ngapi hapo," alisema Profesa Ngowi.

Alisema sehemu nyingine wanapokwama makandarasi wa ndani ni kuhamisha fedha za mradi mmoja kwenda kutekeleza mradi mwingine jambo ambalo halishauriwi kimahesabu kwani mwisho wake huwa mbaya.

Profesa alisema baadhi ya makandarasi hucheza michezo ya hatari zaidi kwa kuwekeza kwenye kilimo fedha walizopata kwaajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi na mwisho wa siku biashara ikiwa mbaya wanashindwwa kukamilisha miradi kwa wakati na kwa ubora waliokubaliana na mwenye mradi.

"Unapopewa fedha za mradi A basi ziwe kwaajili ya mradi A usizipelele kwenye mradi B kwasababu utachanganya hesabu na usione faida na hata unapokamilisha mradi na kubaki na fedha usizihesabu hizo kama faida, kumbuka kuna kodi, marejesho ya benki, kulipa madeni, kununua vifaa kama magreda ili kukuza kampuni," alisema

# Asasi inayoamini ndoa bora ni msingi imara kwa jamii, taifa

Na Mwandishi Wetu

NDOA ni taasisi kongwe kuliko zote tangu kuumbwa kwa ulimwengu. Ni jambo ambalo Mungu aliagiza mwanamume awe na mwanamke ambao kwa kawaida hawatakuwa wawili tena bali mwili mmoja.

Licha ya Mungu kuwaunganisha watu hao, aliwapa agizo kwamba baada ya kuwa pamoja wakazae, kuongezeka na kuijaza nchi. Zaidi ya hayo aliwapa mamlaka ya kuvitawala viumbe vyote vilivyoko duniani.

Kwa maneno mengine, ndoa ni muungano wa hiari kati ya mwanamume na mwanamke unaokusudiwa kudumu kwa muda wa maisha yao.

Ni wazi kuwa kuoa au kuolewa huwa ni ndoto kubwa kwa watu ambao wako kwenye uhusiano na wana nia ya dhati ya kuishi pamoja ili kujenga familia bora na imara. Lengo kuu la ndoa licha ya kuwa na familia, ni kuwa na mafanikio katika maeneo yote kimaisha.

Wataalamu wanaeleza kuwa ndoa ndiyo njia pekee inayoweza kumsaidia binti au kijana kuwa kwenye uhusiano ambao ni endelevu licha ya kuwa humo ndani wanakumbana na vikwazo mbalimbali.

Pamoja na hayo, katika kizazi cha sasa, ndoa nyingi zimekuwa zikivunjika na kusambaratika kwa kile kinachodaiwa kwamba wanandoa kushindwa kuvumiliana na kuchukuliana katika mambo mbalimbali.

Kutokana na hali hiyo, kumekuwa na ulazima kwa jamii kuingilia kati ili kunusuru ndoa na athari zitokanazo na ndoa kusambaratika. Katika kufanya hivyo, asasi ya Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare) imejitosa kushughulikia changamoto hizo baada ya kugundua changamoto nyingi katika uhusiano, ndoa na malezi ya watoto.

Mkurugenzi Mtendaji na mwasisi wa TaMCare, Mchungaji Dk. Enock Mlyuka, anasema asasi hiyo imeanzishwa ili kutoa huduma bora na endelevu kuhusu masuala ya ndoa, familia na malezi bora kwa watoto, lengo likiwa ni kujenga familia na jamii bora kwa maendeleo ya taifa kwa ujumla.

**SABABU NI NINI?**

Kwa mujibu wa Dk. Mlyuka, asasi hiyo amebainisha kuwa ziko sababu tatu ambazo zinachangia ndoa nyingi nchini kuvunjika ikiwamo ya watu kukosa umakini wakati wanapofanya uamuzi wa kutaka kuoa au kuolewa.

Dk. Mlyuka anasema sababu nyingine ni kukosekana kwa ufahamu na maarifa ya kutosha kuhusu taasisi hiyo muhimu pamoja na malezi mabaya wakati wa utoto ambayo yamekuwa yakiathiri makuzi.

"Wanandoa wengi sasa hivi wanashindwa kuishi maisha ya ndoa. Wengi wao wamekuwa wanaharakati zaidi katika ndoa kuliko kuwa walezi hali ambayo imesababisha migogoro na kuvunjika kwa ndoa nyingi, " anasema na kuongeza:

"Watu wengi wanaingia kwenye ndoa bila kupata elimu na mafunzo ya kutosha matokeo yake sasa hivi tuna idadi kubwa ya ndoa zinazovunjika."

Taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria iliyotolewa bungeni mwaka jana, ilibainisha kuwa idadi ya ndoa 26,953 na talaka 122 zilisajiliwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA).

Hata hivyo, Dk. Mlyuka alisema kwa mujibu wa takwimu hizo, ila mwezi kuna wastani wa talaka 14 zilizosajiliwa nchini sawa na talaka moja kila baada ya siku mbili.

Hatua hiyo, alisema inarudisha nyuma maendeleo na ustawi wa familia, jamii na taifa kwa ujumla kwa kuwa ndoa ni kitovu cha familia na malezi huku akisisitiza kuwa kama taasisi hiyo muhimu (ndoa) itakuwa imara, basi tutakuwa na jamii na taifa imara.

Kwa msingi huo, anasema TaMCare iameamua kuanzisha mafunzo ya kina kuhusu ndoa kwa wanandoa na wanandoa watarajiwa.

Sambamba na hayo, anasema taasisi hiyo inatoa mfunzo ya ndoa na uhusiano katika maeneo ya kazi. Kwa kuanza, taasisi hiyo imetoa mafunzo hayo kwa walimu wa shule ya Sekondari ya Zinga, Bagamoyo mkoani Pwani.

Halikadhalika, anabainisha kuwa TaMCare imeelekeza nguvu zake katika kuwasaidia wazazi wasio na wenza (single mothers) hasa wale wanaoishi katika mazingira magumu na wenye hali duni ya maisha.

"Tumewatembelea wanawake wasio na wenza wapatao 505 mjini Bagamoyo na wengi wao bado ni vijana, ambao ni nguvu kazi ya Taifa.

Tuna mipango ya kuwasaidia baada ya kugundua kuwa wengi wao wanaishi na kulea watoto wao katika mazingira magumu hali inayoathiri afya na makuzi ya watoto hao. Tunaamini kuwa, kwa kuwasaidia wanawake hawa, tutakuwa tumewasaidia watoto hao", anasema.

Anasema idadi ya watoto wanaotunzwa na kulelewa na wanawake hao ni takribani 1543 ambapo wengi wao wameachika na kutelekezwa na wenza wao . "Wanawake hawa wanafanya biashara ndogondogo ili kujikwamua kimaisha na watoto wao, kimsingi wana hali duni," anasema.

Anasema wanajipanga kuwasaidia wanawake hao baada ya kugundua kuwa wengi wao wameathirika kisaikolojia, wamekata tamaa ya maisha pia ni kundi ambalo limesahaulika katika jamii.

Katika kuhakikisha taifa linakuwa na nguvu kazi bora, yenye maadili na inayojitambua, asasi hiyo imeanza kutoa elimu ya stadi za maisha kwa wanafunzi wa sekondari na vyuo.

Mafunzo hayo, anasema yanalenga pia kuwasaidia kujitambua na kuwa raia wema wenye nidhamu, wenye kujua kujitawala, wenye kujiamini, wenye kuwajibika ipasavyo, na wenye kujua namna ya kukabiliana na changamoto mbalimbali za maisha.

**FALSAFA YA ASASI**

Pamoja na kujikita katika program hizo, Mkurugenzi huyo anasema ukosefu wa fedha ni tatizo si kwa TaMCare tu bali kwa asasi mbalimbali za kijamii katika uendeshaji na utekelezaji wa majukumu. Kutokana na hali hiyo, wanafanya shghuli zao kwa kujitolea zaidi.

"Falsafa yetu ni kwamba fedha zikute mipango na kazi zikiendelea na si kusubiri fedha. Zikija huduma zetu kwa wananchi zitapanuka zaidi na wananchi kunufaika.

Kutokana na falsafa hiyo, Dk. Mlyuka anasema wamepata mafanikio tangu kuanzishwa ikiwa ni pamoja na kuwa na ofisi iliyoko Bagamoyo, kukamilisha nyaraka muhimu za kiutawala na uendeshaji na pamoja na mpango mkakati wa miaka mitatu (2020-22), ambao ulizinduliwa hivi karibuni.

"Katika kutekeleza mipango yetu, tumeanza kutoa mafunzo ya ndoa na elimu ya stadi za maisha kwa wanafunzi pamoja na kukutana na wanawake wasio na wenza wanaoishi katika mazingira magumu ili kuandaa mradi wa kuwasaidia.

"Katika kutekeleza majukumu yetu kwa jamii, asasi ya TaMCare inafanya kazi zake kwa kushirikiana na serikali, taasisi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na taasisi za dini," anasema na kuongeza:

"Tunatoa mafunzo mahususi kuhusu taasisi ya ndoa kwa wanandoa na vijana wa kike na kiume wanaotarajia kuingia kwenye ndoa, kutoa msaada wa kisaikolojia, elimu ya uzazi, malezi na ujasiriamali kwa wazazi wasio na wenza (single mothers) hasa wanaoishi katika mazingira magumu.

Pia taasisi hiyo inatoa ushauri nasaha wa uhusiano kwa vijana, wanandoa, kuandaa na kufanya semina na makongamano ya jinsi ya kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia , unyanyasaji, mimba na ndoa za utotoni.

"Pia tunafanya utafiti, tunaandaa, kuchapisha na kusambaza vielelezo na machapisho mbalimbali yenye lengo la kuelimisha jamii kuhusu ndoa na familia, malezi na haki za watoto. Tunatoa mbinu shawishi (advocacy) kwa serikali na vyombo mbalimbali vinavyohusika ili kufanya maboresho katika Sheria, Sera na miongozo kwa lengo la kuimarisha ndoa na familia," anasema.



Mchungaji Dk. Enock Mlyuka



WANAFUNZI wa sekondari wakiwa katika mafunzo ya stadi za maisha. **PICHA: TaMCare.**

# Mtu aliyeua watatu Ufaransa atambuliwa

**PARIS, Ufaransa**

MTU aliyefanya shambulizi na kuua watatu ndani ya kanisa nchini Ufaransa, imetambuliwa kuwa mhamiaji kutoka Tunisia.

Mtuhumiwa huyo Brahim Aouissaoui (21), ambaye alipigwa risasi na polisi baada ya shambulizi hilo, alikutwa na nyaraka za Shirika la Msalaba Mwekundu la Italia, ambazo alipewa mara alipowasili kisiwa cha Lampedusa kwa kutumia boti la wahamiaji mwezi uliopita.

Hata hivyo, mtu huyo kwa sasa amelazwa katika Hospitali moja akiwa katika hali ya mahututi.

Katika tukio hilo lilotokea siku ya Alhamisi wiki hii, mtu huyo aliwashambulia kwa visu waumini wakati wakiwa ndani ya kanisa la Notre-Dame balisica mjini Nice.

Mmoja wa waathiriwa wa shambulio la kuchomwa kisi siku

Rais wa nchi hiyo, Emmanuel Macron, alisema shambulio hilo lilikuwa la kigaidi.

Rais Macron alisema idadi ya polisi imeongezwa kutoka 3,000 hadi kufikia 7,000 kwa ajili ya kutoa ulinzi katika maeneo ya umma kama vile makanisa na shule. Waendesha mashtaka wa kukabiliana na ugaidi, walianzisha uchunguzi wakati serikali ikiimarisha usalama.

Tukio hilo limezidi kuwapa hofu raia wa Ufaransa baada ya shambulio lingine kama hilo kutokea mapema mwezi huu karibu na shule moja kaskazini magharibi mwa mji wa Paris, na kusababisha mwalimu Samuel Paty, kuawa kwa kukatwa kichwa kufuatia kitendo chache cha kuwanyesha wanafunzi vikaragosi vyenye utata kuhusu Mtume Muhammad.

Mshukiwa huyo alisikika akisema kwa sauti maeneno "Allahu Akbar" (Mungu ni mkubwa) mara kadha kabla ya kupigwa risasi na polisi.

Mkuu wa waendesha mashtaka wanaokabiliana na ugaidi wa Ufaransa, François Ricard, alisema baada ya kumpekua alikutwa na nakala ya Quran, simu mbili na kisu cha inchi 30.

"Pia tulipata begi lililoachwa na mshambuliaji huyo, kanda na visu viwili ambavyo havitumiwa," aliongeza.

**BBC**



Kikosi cha polisi wanaopambana na ugaidi wa Ufaransa, wakifanya upekuzi katika kanisa la Notre-Dame Balisica, mjini Nice baada ya watu watatu kuuawa na mshambuliaji aliyejihami kwa kisu juzi. **(PICHA: AFP)**

# Maelfu waandamana Georgia

**TBILISI, Georgeia**

MAELFU ya waandamanaji wanaounga mkono upinzani nchini Georgia, wameingia mitaani kuipinga serikali ya nchi hiyo.

Maandamano hayo yanafanyika siku mbili kabla ya kufanyika uchaguzi wa wabunge.

Rais wa zamani wa nchi hiyo, Mikhail Saakashvili, aliwahutubia waandamanaji hao waliokusanyika katika viwanja vya uhuru katika mji mkuu wa nchi hiyo, Tbilisi, akiwa nchini Ukraine, ambako anaishi kama mkimbizi. Matokeo ya kura za maoni yanaonyesha serikali ya chama cha Georgian Dream, kinachoongozwa na bilionea Bidsina Ivanishvili, inaweza kushindwa kwa kura chache katika uchaguzi huo utakaofanyika leo.

Hata hivyo, chama cha upinzani cha United National Movement, kitahitaji kuungana na vyama vingine ili kuing'oa madarakani serikali ya Ivanishvili.

**DW.**

# Ujerumani kuendelea kuweka majeshi Iraq

**BERLIN, Ujerumani**

UJERUMANI imerefusha muda wa wanajeshi wake kuendelea kukaa Iraq, kwa muda wa miezi 15 zaidi.

Bunge la shirikisho la nchi hiyo, Bundestag, limekubali kurefusha muda ujumbe wa kijeshi wa nchi hiyo kufanya kazi nchini humo mpaka Januari mwaka 2022.

Hata hivyo, Bunge hilo lilipunguza idadi ya wanajeshi, kutoka 700 hadi 500.

Uamuzi huo uliopitishwa juzi na kuungwa mkono na wabunge 431.

Majukumu ya wanajeshi wa Ujerumani nchini Iraq, ni kutoa mafunzo ya kupambana na kundi linalojiita Dola la Kislamu, IS.

**DW**

# Mpango wa kuondoa wanajeshi DRC wajadiliwa

**NEWYORK, Marekani**

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, amependekeza mpango maalum ambao utatumika kuwaondoa hatua kwa hatua wanajeshi wa kulinda amani Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mpango huo unaeleza baada ya kuwaondoa wanajeshi hao wanaolinda amani nchini humo, majukumu ya usalama yatakabidhiwa kwa serikali.

Katika waraka wa kurasa 15, alioliandikia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, Guterres alisema ujumbe wa Umoja wa Mataifa umekubaliana na serikali ya DRC juu ya mkakati huo, katika mkutano uliofanyika tarehe 19 Oktoba mwaka huu.

Aliongeza kuwa pande hizo zitaendelea kujadiliana kuhusu namna ya kuweka mazingira yatakayowezesha kuondoka kwa ujumbe huo.

Katibu mkuu huyo alisema ikiwa baraza litauridhia, Umoja wa Mataifa utaandaa mpango wa mpito, unaozingatia vigezo vya tathmini ya athari zinazoweza kuambatana na zoezi hilo.

**DW**

# Vita yaivuruga Nagorno-Karabakh

**STEPANAKERT, Nagorno**

MAOFISA katika jimbo lililojitenga la Nagorno-Karabakh, wamesema vikosi vya Azerbaijan, vimefanya mashambulizi makali katika eneo hilo tangu mgogoro huo uanze.

Ripoti hizo zimeeleza mji mkuu wa jimbo hilo, Stepanakert ulishambuliwa mfululizo kwa saa kadhaa na kusababisha watu kukimbia makazi yao.

Jimbo hilo lenye wakazi wengi wa jamii ya Armenia, limejitangazia uhuru kutoka Azerbaijan, lakini uhuru huo hautambuliwi na taifa lolote duniani.

Wadadisi wa mambo wanahofu kuwa mzozo wa sasa kati ya Azerbaijan na Armenia, unaweza kugeuka vita vya kutumia wanajeshi kutoka mataifa mengine ya Urusi inayoiunga mkono Armenia, na Uturuki ambayo ni mshirika wa jadi ya Azerbaijan.

**DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

Nipashe

NIPASHE NI JIBU LAKO


NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Nipashe


Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**ALOYS SIMON**
amepotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1458.0035.2013** kilichotolewa na shule ya secondary **KIBOGORA** mwaka **2013**,yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/MAG/RB/764275/2020**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MIRIAM LUCAS**
Amepotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0546.0098** kilichotolewa na shule ya secondary **PAMBA** mwaka **2010** ,yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DSM/PHQ/RB/764067/2020**

## KUPOTEA KWA PASSPOTI



115967802

**AMINA SELEMANI MKUMBI** Amepotelewa na PASSPOT ya kusafiria yenye namba **TAE 293859** iliyotolewa mwaka 2020, yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/KIL/RB/764783/2020**

## KUITWA SHAURINI MDAIWA

**Mahakama ya Mwanzo MAKOLE**
**Wilaya ya DODOMA - MJINI**
**MADAI NAMBARI 29 YA 2020**

Mdai: **ZULFA ELZEI MAKASO**
DHIDI YA
Mdaiwa **ALLY YUSSUPH FAKI**
Kwa: **ALLY YUSSUPH FAKI – DAR ES SALAAM.**
Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta/madai yake/yao kwamba
**MADAI YA TALAKA**
Kwa hiyo unahitajika/mnahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe **10/11/2020** siku ya **JUMANNE** saa **2:30** asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo, lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo. Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **27/10/2020.**

## USIMAMIZI WA MIRATHI

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**FORM II**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA)**
Katika Mahakama ya **MJINI PANGANI**
Usimamizi wa Mirathi Na. **13/2020**
Ombi la **KOMBO ALLY NYANGE** kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **FATUMA NONDO**
Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII.
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **07/12/2020** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo. Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
Tarehe **26/10/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**Jimbo Katoliki la Rulenge Ngara,** linatangaza kupotelewa na kadi za gari. Kadi ya Gari namba **T 112 BFB** aina ya Mitsubishi Pajero yenye chassis namba **V4642000831**
Kadi ya Gari namba **T 470 AKH** aina ya Toyota Hilux double Cabin yenye chassis namba **JTFDI 626900083023**
Kadi ya Gari namba **T 312 AKH** aina ya Isuzu Canter yenye Chassis namba **JAANPR 66LX1038918**
Yeyote atakayezipata awasiliane na mhusika kwa namba **0684960607** au kituo chochote cha polisi kilicho karibu yake. Taarifa ya polisi: **GEI/CHA/RB/759007/2020.**

115970102

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**JUDICIARY IN THE HIGH COURT OF TANZANIA AT BUKOBA**

**LAND CASE APPEAL NO. 61/2018**

(Arising from land appeal no 13/2017 at district land and housing tribunal of Muleba at Muleba originating from land case no 119/2017 and land case no 110/2011 and appeal no 13/2017 at the district land and housing tribunal for Kagera at Bukoba)

**COSTANCIA KAMUGISHA ………………………………APPELLANT**

**VERSUS**

**BERNARD LUTASHABA…………………………RESPONDENT**

**TO BERNARD LUTASHABA**

**RE: NOTICE OF DATE OF MENTION**

Whereas the above mentioned Appellant lodged Appeal against you and registered as land case appeal no 61/2018

Take Notice that the above said Appeal has been fixed for mention on **7th December 2020 at 8:30 Am** before **Hon. N.N. KILEKAMAJENGA** Judge you are ordered to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said hearing the case will proceed in your absence.

Given under my hand and seal of this Court this 27th day of October, 2020.

J.M. Minde
DEPUTY REGISTRAR
BUKOBA

115969202

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MAJID SALIM ALLY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina TOYOTA DYNA yenye namba za usajili **T 937 ANP.** Chassis no. **YY510006335,** Engine no. **2Y056762.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/761981/2020.**

115970002

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# Mauaji Harusini-**36**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

"Umesema unaitwa George Kupila si ndiyo?"

"Sawa Kabisa."

"Okay, mimi sina mengi sana. Ila ningependa nikuulize swali moja tu."

George hakujibu kitu, badala yake sura ilionekana kutaka swali liulizwe.

"Unamfahamu Timo?"

"Timo yupi?"

"Kijana mmoja msela hivi ambaye alipewa kazi ya kumuua Fikiri."

Kwa mbali Eddy alihisi mshtuko kwenye moyo wa George.

Macho yalimtoka pima na mapigo ya moyo yakaongezeka.

Eddy alikuwa na uzoefu na mambo hayo, hivyo aliona hali isiyo ya kawaida kwenye uso wa George.

Awali aliambiwa aripoti kwenye Kituo Kikuu cha Polisi, baada ya kuambiwa gari lake lilikuwa na makosa ya usalama barabarani. Haikuwa hivyo. Eddy aliamuru hivyo, baada ya kubainika kuwa gari hilo ndilo lililokuwa na mtu ambaye alikuwa na Timo, muda mfupi tu kabla ya kifo cha Fikiri.

Timo ambaye yupo kizuizini alieleza yote baada ya kupata kibano.

George ambaye ndiye mmiliki wa gari alipofika hapo kituoni, askari alimpigia simu Eddy ambaye alimtuma mmoja wa wafanyakazi wa ofisi yake kwenda kumchukua kumpeleka kwenye ofisini mwake.

"Timo huyo huyo unayemfahamu wewe."

"Simjui mimi huyo."

"Sawa, hilo tutalijua." Eddy alinyanyua simu na kumwita mmoja wa wafanyakazi.

"Mlete yule jamaa yetu tuliomuweka ndani majuzi."

Baada ya dakika mbili mlango ulifungiliwa na mfanyakazi huyo aliingia na Timo.

George alionekana kupatwa na mshtuko alipomuona.

"Timo, umekaa ndani inakaribia wiki sasa. Sasa kama unataka kwenda uraiani, hebu niambie huyu unamfahamu?"

"Ndiyo."

"Ni nani?"


"Jina simjui, lakini huyu ndiye aliyenipa pesa na kunituma nimuue Fikiri."

"Una uhakika kuwa ni huyu?"

"Nina uhakika kwa sababu hatukuonana siku moja. Siku ya kwanza tulionana na siku ya pili pia tulionana, siwezi kumpotea."

"Unasikia bwana George, huyu atakuwa ndiye shahidi kwenye kesi yako tutakapokwenda mahakani, kwa hiyo sina shaka na hili. Swali langu la pili ni kwa nini ulitaka Fikiri auawe?"

George, aliyeonekana kuwa na umri wa miaka 30 hivi, mwembamba na mrefu, alionekana kufikiria sana.




**Sasa nataka kitu kimoja. Utusaidie ili ndugu zako wote hao wapatikane. Na ikiwa hivyo unaweza kupata unafuu wa adhabu. Badala ya kukupa mashataka ya kujaribu kuua kwa makusudi kama wenzako, wewe naweza kuwaambia wakufungulie mashtaka ya kujaribu kuua bila kukusudia. Sawa?**

"Kumbuka mtu uliyemtuma kumuua Fikiri ndiyo huyu hapa. Ukikataa ni kujitafutia matatizo." Eddy alikumbusha.

"Alinidhulumu pesa zangu." Alijibu baada ya kufikiria sana.

"Mtu akikudhulumu, unamdai na kumpeleka kwenye vyombo vya sheria, au unamuua?"

"Hakutaka kunilipa kabisa na akawa ananitukana. Isitoshe pia akanichukulia mpenzi wangu."

"Tuelewe nini hapa. Unamdai, au kakuchukulia mpenzi wako?" Eddy aliuliza.

Wakati huo Eddy alikuwa akirekodi maelezo hayo, huku msaidizi wake akiyaandika kwenye daftari.

"Namdai na kanichukulia demu."

Eddy alinyanyuka kitini na kutoka kidogo kiasi cha dakika tatu hivi. Aliporejea kila mtu alikuwa anamtazama alitoka kwenda wapi na anarudi kufanya nini.

Kabla hajakaa aliweka kitu kilichofungwa na karatasi mezani. Kila mtu alishangaa. Ndani ya ofisi hiyo kulikuwa na watu wanne. Eddy mwenyewe, msaidizi wake, Timo na George.

Kilichowashangaza wengi ni kwamba wakati anarejea alikuwa amevaa 'glovu' mkononi.

Alikaa kwenye kiti na wote macho yao yalielekezwa kwenye meza. Hakuna aliyejua nini anafanya, anakusudia au kitu gani kilichowekwa.

Alianza kufungua karatasi kwa uangalifu mkubwa. Karatasi ilipotolea, kilibaki kifuko kidogo cha plastiki.

Kuna kitu kiliwekwa humo, lakini kilikuwa nusu.

Macho ya Eddy kwa uangalifu yalimtazama George ambaye alionekana kushtuka isivyo kawaida.

Macho yalimtoka pima. Mapigo ya moyo yaliongezeka. Haraka aligauza kichwa chake na kuangalia pembeni.

Eddy alitabasamu. Halikuwa tabasamu halisi. Alichodhania ndicho kilichotokea.

"Unakijua kuna nini humo?"

Hakuna mtu aliyejibu kwa sababu hakuna mtu aliyejua nani anaulizwa kati yao.

"Nakuuliza George, ndani ya hiki kifuko kuna nini?"

"Sijui?" Alijibu kwa tabu, huku sauti ikionekana kukwamakwama.

"Timo unajua humo ndani ya kifuko hicho kuna nini?"

"Sujui bwana mkubwa."

"Hiyo ni sumu." Eddy alijibu na kuwaangalia wote kwa zamu. Kila mmoja alishangaa kwa namna yake.

"Sumu hiyo ilikusudiwa kumuua msichana mmoja hivi. Huyo msichana alikuwa ana tabia ya kwenda ABC Hotel maeneo ya Mbezi Beach kila Jumamosi kula chakula cha mchana. Iliwekwa kwenye chakula chake. bahati mbaya aliyeweka aliangusha kifuko hiki. Wamaria wema wakakiokota na walimjua aliyeangusha. Kikaenda kupimwa ikaonekana kuwa ni sumu. Wakati askari polisi wakimsaka Fikiri, kabla hajamkamata walipata taarifa ya kuuawa." alisema Eddy.

Timo ndiye alionekana kushangaa zaidi, kwani ilionekana kuwa kwake ni habari mpya.

"Sasa nadhani Timo wewe ulitumwa kumuua Fikiri kwa sababu tu ya walitaka afe, hawakutaka aingie kwenye mikono ya polisi, kwani wangempa msukosuko na kuwataja. Umeingia kwenye kesi isiyokuhusu.

Sasa kama George ndiyo alikutuma, nadhani yeye anaufahamu vizuri mchezo huu." Macho ya Eddy yalitua kwa George ambaye ni kama alikuwa nusu mfu. Macho yalimtoka na pamoja na ndani kuwa na kiyoyozi, lakini jasho lilimmiminika.

"George Kupila, unamfahamu dada mmoja anaitwa Shani Patiyo Kupila?" Eddy alibandika nyundo nyingine.

Swali hilo lilionekana kuendelea kumchanganya George. Sasa alijua kila kitu kiko hadharani na hakuwa na njia nyingine yoyote ya kuepuka hilo. Aliona ni bora tu yaishe, kwani kuzidi kukataa kungeendelea kumpa mateso kama ambayo amekuwa akiyapitia tangu alipokamatwa.

"Namfahamu ni mtoto wa marehemu kaka yangu Patiyo."

"Kwa nini mnataka kumuua binti yenu?"

George alikaa kimya na kutafakari. Alikuwa kama mtu anayesali hivi. Baada ya dakika tano aliinua macho.

"Nisamehe bwana mkubwa, ngoja niseme kitu ambacho kitarahisisha yote haya."

Maneno hayo yalimshangaza Timo na msaidizi wa Eddy, lakini mwenyewe Eddy alijua kuwa George atazunguka, lakini hakuna na ujanja kama ni kweli amefanya hivyo. Na kama si kweli, basi atakuwa anamjua mtu ambaye yuko nyuma ya hayo yote.

"Tatizo hapa ni mali tu. Kuna baadhi ya ndugu zangu baada ya kifo cha Patiyo ambaye alikuwa na mali nyingi na makampuni, waliona hakuna haja ya kuwambia binti mali, kwani mama yake mzazi alifariki wakati bado mdogo. Kwa maana hiyo mali ile ni yake. Kaka yetu mkubwa anaitwa Jim, ndiye aliyetuita na kupanga mkakati wa kumuua Shani ili mali zile sasa zote zitahamia kwetu kwa sababu hakutokuwa na mrithi nwingine yoyote, kwani binti ni mtoto pekee wa marehemu." Alisema Gaorge na kushusha pumzi kana kwamba ameutua mzigo mzito.

"Mpango huu ulianza kabla ya kifo cha Patiyo au baada?"

"Kwa sababu nimeamua kukueleza ukweli, bado nitaendelea kueleza ukweli. Ilikuwa ni baada ya kifo cha Patiyo."

"Hamkuhusika kumuua Patiyo ili baadaye mfanye hivyo kwa binti yake?"

"Hapana." Alisema George akionekana kuwa na uhakika na anachokisema.

"Sisi hatukuhusika ni njama za kumuua Patiyo na mkewe wakati wakifunga ndoa. Wazo la kumuua Shani lilikuja baada ya ndugu yetu kufariki na hii ni baada ya mazishi, kikao cha familia, halafu kaka yetu Jim aliitisha kikao cha sisi tu wanaume na kutueleza mpango huo."

"Kwenye mpango huo mlikuwa wangapi?"

"Wanne, kaka yetu Jim, mimi, Paul na Ben."

"Sasa nataka kitu kimoja. Utusaidie ili ndugu zako wote hao wapatikane. Na ikiwa hivyo unaweza kupata unafuu wa adhabu. Badala ya kukupa mashataka ya kujaribu kuua kwa makusudi kama wenzako, wewe naweza kuwaambia wakufungulie mashtaka ya kujaribu kuua bila kukusudia. Sawa?"

"Sawa."

"Hebu nisaidie kitu kimoja, kwa nini hamkutumia risasi kumuua Shani, mkataba kutumia sumu, tena inayoua taratibu?" Eddy alimrudia tena George kwa maswali.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# KOULIBALY AFUNGUKA HAJUI HATIMA YAKE




**NAPLES,** Italia

KALIDOU Koulibaly amesisitiza anaipenda Napoli, lakini afunguka "tutaona nini kitatokea" wakati huu kukiwa na uvumi kuhusu majaliwa yake klabuni hapo.

Koulibaly mwenye umri wa miaka 29, mara kwa mara amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kwa miamba hao wa Serie A, huku Liverpool ikiripotiwa kumwania mlinzi huyo.

Beki huyo wa kati wa kimataifa wa Senegal, ambaye mkataba wake na Napoli unamalizika mwaka 2023, anatambua namna anavyoihitaji, lakini amesema anaipenda klabu hiyo ya Italia.

"Naipenda Naples na watu wa Naples wananipenda mimi, hilo ndio jambo muhimu zaidi," amesema Koulibaly kupitia Sky Sport, baada ya timu yake kushinda bao 1-0 dhidi ya Real Sociedad kwenye Ligi ya Europa.

"Mara zote ninakuwa tayari katika kila mchezo, bado nina mkataba wa miaka mitatu, nimetulia, timu zinaniwania mimi, lakini bado nipo hapa.

"Nacheza katika kiwango changu cha juu na kuisaidia timu na watu hawa kwa sababu nataka kuwapa kitu fulani wao, halafu tutaona nini kitatokea."

# Fabinho atemwa kikosi cha Brazil

**LIVERPOOL,** England

KIUNGO wa Liverpool, Fabinho ameachwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Brazil kwa ajili ya mechi zinazokuja za kuwania kusaka tiketi ya kushiriki Kombe la Dunia na nafasi yake imechukuliwa na Allan.

Fabinho, anatumika kama mlinzi wa kati na kocha Jurgen Klopp baada ya Virgil van Dijk na Joel Matip kuumia, naye aliumia misuli kweye mchezo wa Liverpool wa ushindi wa mabao 2-0 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Midtjylland, Jumanne.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 ataikosa Brazil katika mechi zake dhidi ya Venezuela na Uruguay mwezi ujao, na ilithibitishwa Allhamisi.

Kiungo wa Everton, Allan, ambaye amecheza mechi tisa kwa Brazil, amechukua nafasi ya Fabinho kwenye kikosi hicho.

"Benchi la ufundi la kikosi cha Brazil limemwita kiungo Allan, kutoka Everton ya England, kwa ajili ya mechi mbili za kufuzu Kombe la Dunia mwaka 2022," ilisomeka taarifa ya Shirikisho la Soka la Brazil (CBF).

Brazil inaongoza kwenye kundi lake la kufuzu baada ya kushinda mechi mbili za ufunguzi na sasa itaanza kukutana na Venezuela, Novemba 13, mwaka huu.






# Mo Salah kuiongoza Misri kufuzu Afcon

**CAIRO,** Misri

MOHAMED Salah ataongoza kikosi cha wachezaji 19 wa Misri kilichoitwa kwa ajili ya mechi mbili za kuwania kufuzu fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) mwakani kilichotangazwa na Kocha, Hossam El-Badry.

El-Badry ameonekana kutoa kipaumbele kikubwa kwa wachezaji wanaocheza ligi ya nyumbani ambao amewaita 14, huku watano tu wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi hiyo.

Misri itawakabili Togo kati ya Novemba 9 hadi 17, mwaka huu kwenye michuano hiyo ya kufuzu mashindano hayo ya Afrika.

Kiungo wa Arsenal, Mohamed Elneny ni staa mwingine ambaye El-Badry amemjumuisha katika kikosi chake ambacho pia kitakuwa na winga wa Aston Villa, Mahmoud Hassan 'Trezeguet'.

Wengine walioitwa kikosini ni beki Ahmed Hegazi ambaye hivi karibuni amesajiliwa na Ittihad Jeddah ya Saudi Arabia akitokea West Bromwich Albion ya England pamoja na mshambuliaji wa Olympiacos ya Ugiriki, Ahmed Hassan Kouka.

Timu ya Pyramids imeongoza kwa kutoa idadi kubwa ya wachezaji katika kikosi hicho ambapo jumla ya wachezaji nane wameitwa wakitokea kwenye timu hiyo, lakini pia klabu nyingine ambazo zimetoa wachezaji ni pamoja na Zamalek, Al Ahly, ENPPI, El Gouna, Arab Contractors, Tala'a El Gaish na Smouha.

Kikosi kamili cha Misri kinaundwa na El-Mahdy Soliman, Ramadan Sobhi, Abdallah El-Said, Ali Gabr, Ahmed Hegazi (Ittihad Jeddah), Ahmed Ayman Mansour, Mohamed Hamdy, Mohamed Farouk, Ahmed Tawfik (Pyramids FC), Mohamed Bassam (Tala'a El-Gaish)

Wengine ni Mohamed Salah (Liverpool) Mohamed Sherif (ENPPI), Mohamed Elneny (Arsenal), Hossam Hassan, Ahmed Aboul-Fotouh (Smouha), Ahmed Kouka (Olympiacos), Taher Mohamed (Arab Contractors), Akram Tawfik (El-Gouna) na Mahmoud Hassan 'Trezeguet' (Aston Villa).

Misri inashika nafasi ya tatu katika Kundi G la kuwania kufuzu Fainali za Afcon 2021 ikiwa na pointi mbili ilizopata baada ya kucheza mechi mbili ikiwa nyuma ya Comoro inayoongoza kundi hilo ikiwa na pointi nne, Kenya ikiwa nafasi ya pili na pointi mbili huku Togo yenye pointi moja ikishika mkia.

# Solskjaer ajipanga usajili wa Januari

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amesema atafanya usajili katika dirisha dogo la usajili la Januari.

Baada ya kushindwa kufanya usajili mkubwa kwenye dirisha la majira ya joto lililopita, kocha bado mipango yake ya usajili ipo kwa wachezaji wale wale ambao atahitaji kupata huduma zao pale Old Trafford.

United imepanga kufanya biashara ya 'kibabe' usajili wa majira ya kiangazi mwakani kwa kuhakikisha inanasa saini za mastaa straika, Erling Haaland, winga, Jadon Sancho na beki wa kati Dayot Upamecano.

Solskjaer alijaribu kufanya usajili wa Haaland Januari, mwaka huu lakini ikashindikana na staa huyo alitimkia zake Borussia Dortmund.

Hata hivyo, kwenye mkataba wake kuna kipengele kinachohitaji kulipwa pauni milioni 68 pekee kuvunjwa kitu ambacho Solskjaer amepanga kukifanya dirisha litakapofunguliwa.

Haaland alisema: "Solskjaer amekuwa na mchango mkubwa sana katika maisha yangu, kama mwanadamu na kama kocha.

"Alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya na alikuwa mchezaji mahiri. Amenifundisha mambo mengi sana."

Kuhusu ishu ya Sancho, ambaye alihusishwa sana kutua Old Trafford kwenye dirisha lililopita la majira ya joto, kocha wake wa Dortmund, Lucien Favre amedai kwamba tangu dili la winga huyo Mwingereza kushindwa kujiunga na United, kiwango chake kimeshuka ndani ya uwanja.





# KLOPP ATOA NENO KWA WILLIAMS

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema ana kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha anamjenga zaidi, Rhys Williams ili aendelee kuonyesha kiwango cha kuvutia.

Mlinzi huyo alikuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya FC Midtjylland, Jumanne iliyopita.

Williams aliingia dakika ya 30 katika mchezo huo ambao Liverpool ilishinda mabao 2-0, akichukua nafasi ya Fabinho aliyepata majeraha ambayo huenda yakamweka nje kwa muda mrefu.

"Amecheza kwa kiwango kikubwa. Ubaya ni kwamba tuna siku nne za kujiandaa kabla ya kukutana na West Ham," alisema Klopp akinukuliwa na Sky Sport.

Upande wetu tunajaribu kupambana kuhakikisha tunamfanya anatuliza mihemko ili aje kuonyesha kiwango kikubwa."

Mchezaji huyo ni zao la Akademi ya Liverpool na msimu uliopita alikuwa anacheza kwa mkopo huko Kidderminster inayoshiriki madaraja ya chini hapo England na kuonyesha kiwango kikubwa jambo ambalo linamfurahisha Klopp.

# Kikosi cha kwanza Milan chamtesa Pioli

**MILAN,** Italia

KOCHA wa AC Milan, Stefano Pioli, amedai ugumu wa kuchagua kikosi cha kwanza unaongezeka katika timu yake baada ya kushuhudia ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Sparta Prague, kwenye Ligi ya Europa, juzi Alhamisi.

Pioli alifanya mabadiliko matano kwenye kikosi chake kilichotoka sare ya 3-3 na AS Roma kwenye mchezo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, wikendi iliyopita na Milan imepata ushindi wake wa tisa katika mechi 10.

Wawili kati yao ni dira mpya, Brahim Diaz na Diogo Dalot, ambao walifunga, huku pia Rafael Leao aliyetokea benchi alifunga.

Milan itarudi kwenye ligi Jumapili wakati itakapocheza na Udinese na Pioli anasema inamwia vigumu kuchagua wachezaji wa kikosi cha kwanza.


"Timu inajua nini inatakiwa kufanya uwanjani na namna ya kuusoma mchezo," alisema akiiambia Sky Sport Italia.

"Tulitoka kuwa na kiwango sio kizuri dhidi ya Roma na kulazimishwa sare. Lakini leo (juzi) tulitawala mchezo.

"Lazima nikubali, ugumu inazidi kuongeza katika kuchagua kikosi cha kwanza katika timu yangu."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA UL...




# ARTETA AMKUMBUSHA PEPE KUJIIMARISHA

**Aeleza mtazamo wake kuhusu winga huyo kutoka Ivory Coast na kubainisha alifurahishwa...**

**LONDON,** England

MIKEL Arteta anatambua kuwa, Nicolas Pepe lazima kiwango chake kiwe cha mwendelezo, lakini kocha huyo wa Arsenal hana swali kwa mtazamo wa winga huyo na yupo tayari kumsaidia.

Pepe alinunuliwa kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo Agosti, mwaka jana kutoka Lille ya Ufaransa, lakini amekuwa na wakati mgumu wa kuonyesha kiwango chake kama ilivyokuwa wakati akicheza kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, ndani ya Ligi Kuu England msimu huu.

Raia huyo wa Ivory Coast katika msimu wake wa kwanza England alifunga mabao matano tu kwenye ligi, wakati kule Ufaransa alifunga mabao 22 kwa msimu mmoja.

**Pepe alionyesha kiwango cha kuvutia Alhamisi wakati akifunga bao la kwanza kwenye ushindi wa 3-0 katika Ligi ya Europa dhidi ya Dundalk, likiwa bao lake la pili kwa msimu huu mpya kwenye mashindano yote.**

Lakini sasa nyota huyo mwenye umri wa miaka 25 anatakiwa na kocha wake, Arteta kuendelea kuwa na kiwango hicho kwenye Ligi Kuu England.

"Namjua Nico, sidhani kama kuna kitu ambacho kinamfanya awe na hofu sana," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari.

"Ni suala la yeye mwenyewe kuwa kwenye kiwango bora, kila wiki. Naamini hapa ndio sehemu pekee anayofikiri anaweza kuwa bora zaidi na tunajaribu kumsaidia.

"Nafikiri yupo tayari kufanya vizuri na kumwonyesha kila mmoja pamoja na wachezaji wenzake, mimi na mashabiki kwamba yeye ni mchezaji ambaye anaweza kutengeneza tofauti kila wiki.

"Kwa uhakika kabisa hajawa kwenye chaguo la kwanza kwenye mechi nyingi, lakini kwa hakika kabisa amekuwa na nyakati nzuri zaidi za kucheza anapopewa nafasi kuliko wengine.

"Ni suala la kuwa kwenye kiwango mwendelezo na hilo litamfanya apate nafasi za kucheza mechi nyingi zaidi."

## ZISIKUPITE

### GUARDIOLA ATAKIWA BARCA

MGOMBEA urais katika Klabu ya Barcelona, Victor anataka kumrejesha Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola katika klabu hiyo. Guardiola anahudumia mwaka wa mwisho wa mkataba wake pale Etihad. ***(Sky Sports)***

### ALDERWEIRELD KUONDOKA SPURS

MLINZI wa Tottenham Hotspur, Toby Alderweireld, huenda akaihama klabu hiyo mara tu mkataba wake utakapomalizika mwaka 2023, anasema baba mzazi wa nyota huyo wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 31. ***(Teamtalk)***

### LIVER YAMGANDA KOULIBALY

LIVERPOOL bado wanamtaka mlinzi wa Napoli, Kalidou Koulibaly na wanatarajiwa kutangaza dau lingine na la kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal mwenye umri wa miaka 29, Januari mwakani. ***(Calciomercato)***

### WEAH ANUKIA ETIENNE

MSHAMBULIAJI wa Lille na Marekani, Timothy Weah mwenye umri wa miaka 20, huenda akajiunga na Saint-Etienne kwa mkopo. ***(L'Equipe)***

### POCHETTINO ANUKIA UNITED

MLINZI wa zamani Tottenham Hotspur, Jan Vertonghen anaamini kocha wa zamani wa klabu hiyo, Mauricio Pochettino atarudi katika Ligi Kuu England hasa kwenye Manchester United. ***(Star)***

### GUENDOUZI ATOBOA SIRI

KIUNGO wa kati wa Arsenal, Matteo Guendouzi mwenye umri wa miaka 21, amedokeza kuwa wachezaji wenzake, Mesut Ozil na Bernd Leno walimshauri ajiunge na Hertha Berlin kwa mkopo. ***(Kicker via Goal)***

### FABINHO KUREJEA MAPEMA

NYOTA wa Liverpool Fabinho hakuumia sana kama ilivyohofiwa. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 27, atakosa angalau mechi tatu tu. ***(Mirror)***

### JUVE: PILO HAONDOKI

JUVENTUS watabaki na kocha wao, Andre Pirlo, licha ya ukosoaji kutoka kwa chombo cha habari Italia kuhusiana na jinsi klabu hiyo ilivyoanza msimu. ***(Mail)***

### WALCOTT HAENDI KOKOTE

MSHAMBULIAJI wa Everton, Theo Walcott anasema anapania kufanya kazi na kocha wa Southampton, Ralph Hasenhuttl kwa mkataba wa kudumu. Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 31 yuko kwa mkopo wa msimu mzima pale Saints. ***(Liverpool Echo)***

### GIGGS AIPOTEZA UNITED

RYAN Giggs anaamini Manchester United huenda ikakosa kushinda taji la Ligi Kuu England kwa miaka 15 au 20. ***(Metro)***

### LAMPARD AMKUBALI PULISIC

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard amesema hakuwahi kutilia shaka uwezo wa winga wa Marekani, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 22, kufanya vyema katika Ligi Kuu England. ***(ESPN)***

HABARI MICHEZO

## Simba Queens yajiimarisha kiufundi

**Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inaendelea kuwa imara na kutetea taji la Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, uongozi wa Simba Queens ya jijini, Dar es Salaam umewaajiri makocha wapya wawili kwa ajili ya kuwanoa magolikipa wake, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Meneja wa Simba Queens, Selemani Erassy, aliwataja makocha hao wapya waliotua kwenye kikosi hicho ni Sophia Joseph na Anna Joel.

Erassy alisema uamuzi wa kuimarisha benchi la ufundi umelenga kumwongezea nguvu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mussa Hassan 'Mgosi' ambaye msimu uliopita aliiongeza vyema timu yake.

"Msimu uliopita benchi hilo halikuwa na kocha wa makipa na msaidizi, sasa wameleta watu hao kwa ajili ya kuhakikisha wanafika malengo yao ya kufanya vizuri zaidi katika msimu mpya wa Ligi Kuu Wanawake nchini," alisema Erassy.

Aliongeza makocha hao tayari wameshaanza majukumu yao na kikosi cha timu hiyo kimeshaingia kambini kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya unaotarajiwa kufanyika kuanzia mapema mwezi ujao.

## Kagera Sugar, Mtibwa hapatoshi

**Na Saada Akida**

KAIMU Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Vincent Barnabas amesema licha ya kufundishwa na Mecky Maxime, amejiandaa kupata matokeo mazuri watakapokutana na Kagera Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

Barnabas aliliambia gazeti hili kikosi chake kitaingia uwanjani na lengo moja la kuondoka na pointi tatu na amejiandaa kumwonyesha mwalimu wake kwamba anaweza.

Alisema anafahamu mechi hiyo itakuwa na ushindani kwa sababu Maxime aliwahi kuiongoza timu hiyo, hivyo anawajua wachezaji na falsafa nzima ya klabu.

Aliongeza mbali na kufundishwa na Maxime, anafahamu kikosi chake kulingana na wachezaji wengi kupita katika mikono yake, hali hiyo haitakuwa rahisi kwake kupoteza pointi katika mechi hiyo.

"Hii ni mechi ngumu na ushindani mkubwa kwangu kwa sababu Maxime anaifahamu vizuri Mtibwa, amewahi kunifundisha soka kipindi alipokuwa kocha hapa, lakini hicho hakitakuwa kigezo kwetu kupoteza pointi katika mechi hiyo ya ugenini," alisema Barnaba.

Alisema wachezaji wake wako katika hali nzuri na wamejipanga kuendelea pale walipoishia.

Kocha huyo ni miongoni mwa wachezaji ambao wamefundishwa na Maxime wakati alipokuwa anaiongoza Mtibwa Sugar kabla ya kuhamia Kagera Sugar.

# YANGA YASAKA USHINDI WA KWANZA MUSOMA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Yanga inatarajiwa kupambana na Biashara United ya Mara leo, vigogo hao wataingia uwanjani wakiwa na kumbukumbu ya kutoshinda mechi yoyote ile kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara.

**Tangu Biashara United ipande na kuanza kucheza Ligi Kuu, msimu wa 2018/19, Yanga imekuwa ikipata ushindi wake Dar es Salaam tu, lakini hali inakuwa tofauti inapokanyaga uwanja huo ambao umekuwa si mgumu tu kwa Yanga, bali timu nyingi zinazofika hapo.**

Yanga ilikanyaga mara ya kwanza kwenye uwanja huo Mei 10, mwaka jana ikiwa ni Ligi Kuu Bara msimu wa 2018/19.

Katika mechi hiyo, Yanga iliambulia kipigo cha bao 1-0, lililofungwa dakika ya nane ya mchezo na Tariq Seif.

Ikumbukwe kuwa baada ya msimu huo ndipo Yanga ilimsajili 'muuaji' huyo aliyekuwa amekwenda nchini Misri kucheza soka la kulipwa, lakini ilishindikana. Kwa sasa Tariq, anaichezea timu ya Polisi Tanzania na tayari ana goli moja.

Msimu uliopita, 2019/20, Yanga haikufungwa kwenye uwanja huo, lakini pia haikupata dawa ya kushinda, baada ya kutoka suluhu 0-0 dhidi ya wenyeji wao Biashara United, mechi ikichezwa Julai 5, mwaka huu.

Kutokana na rekodi hiyo, mashabiki wa soka wanataka kuangalia kama Yanga itavunja mwiko huo kwa kushinda kwa mara ya kwanza kwenye uwanja huo, au hadithi itakuwa ni ile ile.

Yanga imekuwa ikiifunga Biashara United pale tu inapocheza Uwanja wa Benjamin Mkapa, kwani kwa msimu miwili imeshinda mara zote mbili, ikishinda mabao 2-1 Desemba 8, 2018, msimu wa 2018/19.

Shukrani kwa beki, Abdallah Shaibu 'Ninja' na Heritier Makambo kwa kufunga mabao hayo huku Abdulmajid Mangalo akipachika wavuni goli kwa upande wa Biashara United bao la kufutia machozi, na msimu uliopita Desemba 30, 2019, ilishinda bao 1-0 lililofungwa na Tariq, wakati huo akiwa ameshajiunga na Yanga.



Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Oppa Clement (kulia) na beki, Esther Mabanza, wakiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa na mashindano ya COSAFA yatakayofanyika kuanzia Novemba 3 hadi 14, mwaka huu nchini Afrika Kusini. **PICHA: TFF**

# *Msuva ajichimbia Dar akijifua kivyake*

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa Difaa El Jadida na Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Simon Msuva, yuko nchini akiendelea kujifua kwa ajili ya mechi ijayo dhidi ya Tunisia pamoja na maandalizi ya kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Morocco, imefahamika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Msuva ambaye ni winga wa zamani wa Yanga, alisema alibakia nchini kwa sababu ya kujiimarisha kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Morocco hapo Desemba.

Msuva alisema aliona hapa nchini ni mahali sahihi kwake kujiimarisha na itakuwa rahisi kuungana na nyota wengine wa Taifa Stars kwa ajili ya mechi inayowakabili dhidi ya Tunisia itakayochezwa Novemba 13, mwaka huu nchini Tunisia.

"Bado nipo nchini, lakini naendelea kujiweka fiti, nafanya mazoezi kwa sababu kuna mechi ya Timu ya Taifa dhidi ya Tunisia inakuja, halafu nataka hata nikirudi kwenye klabu yangu nisianze upya.Unajua kwa sasa Morocco ligi bado kabisa hadi Desemba ndiyo maana nimebaki nchini," alisema Msuva.

Aliongeza kuwa bado ana mkataba na klabu hiyo akiwa ameshatumikia mwaka mmoja, lakini tayari ameanza kupokea ofa kutoka katika timu nyingine za ndani na nje ya Morocco pamoja na Ulaya.

"Nilisaini miaka mitatu, baadaye nikasaini mwaka mmoja, huo ulikuwa na kipengele cha kuuzwa na ndiyo uliobaki, kwa hiyo ni kweli ofa nyingi zimeanza kumiminika, Watanzania niombeeni dua tu nizidi kusonga mbele," Msuva alisema.

Aliongeza viwango vya wachezaji wengi msimu uliomalizika vilionekana kushuka kutokana na kuwapo kwa virusi vya COVID-19.

# Michezo

Jumamosi Oktoba 31, 2020

Nipashe





Arteta amkumbusha Pepe kujiimarisha UKURASA 22




Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla (kulia), akimkabidhi jezi ya klabu hiyo Mama Maria Nyerere baada ya kwenda kutembelea kaburi la Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere Kijiji cha Butiama, Musoma jana. **PICHA: MTANDAO**

## Fabinho atemwa kikosi cha Brazil

**LIVERPOOL,** England



KIUNGO wa Liverpool, Fabinho ameachwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Brazil kwa ajili ya mechi zinazokuja za kuwania kusaka tiketi ya kushiriki Kombe la Dunia na nafasi...

HABARI UK. 20

## Klopp atoa neno kwa Williams



**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema ana kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha anamjenga zaidi, Rhys Williams ili aendelee kuonyesha...

HABARI UK. 21

# Simba, Yanga kujiuliza Bara

**Na Somoe Ng'itu**

## ● ● ● Vigogo hao wanashuka kwenye viwanja viwili tofauti kuendelea na mbio za kuwania taji...

VITA ya kuwania pointi tatu muhimu katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea tena leo kwa mabingwa watetezi, Simba kuwakaribisha Mwadui FC kwenye Uwanja wa Uhuru wakati Biashara United ikiwaalika Yanga kwenye Uwanja wa Karume Mjini Musoma, mkoani Mara.

**Simba itashuka dimbani leo ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza mechi mbili mfululizo wakati Yanga yenye kocha mpya imeendelea kuwa na rekodi nzuri ya kutopoteza mchezo hata mmoja tangu msimu huu ulipoanza Septemba 6, mwaka huu.**

Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, ameliambia gazeti hili amewataka wachezaji wake wawe watulivu katika mechi ya leo na kusahau matokeo mabaya ya mechi mbili zilizopita ili kuhakikisha wanarejea kwenye mbio za kutetea ubingwa wanaoushikilia. Sven alisema wamejiandaa vyema kuelekea mchezo wa leo na amewakumbusha ni muhimu kuangalia mechi za mbele na 'kupotezea' matokeo ya mchezo uliopita kwa sababu ya kujiimarisha kwenye kufikia malengo.

Kocha huyo alisema anajua mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa sababu wapinzani wao pia wataingia uwanjani wakiamini wanaweza kuifunga Simba kama walivyofanya katika msimu uliopita au timu nyingine.

"Itakuwa mechi ngumu, na si hii tu, michezo yote tunayocheza ni migumu na ina ushindani, sisi ni mabingwa watetezi hivyo kila mmoja anapima ubora wake kupitia timu yetu, tumejipanga kupambana kurejea kwenye malengo yetu," Sven alisema.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema jana bado anaamini kikosi chao kiko kwenye nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara msimu huu licha ya kupoteza mechi mbili mfululizo.

Manara alisema wamejipanga kurejea na ushindi wa kishindo katika mchezo wa leo baada afya ya baadhi ya nyota wao tegemeo waliokosekana kwenye mechi zilizopita kuimarika na kuwa tayari kwa mapambano.

"Nitakuwa mtu wa mwisho kuamini Simba haitachukua ubingwa tena msimu huu, naendelea kuamini tena na tena kwamba tuna kikosi bora kuliko timu nyingine yoyote katika taifa hili na najua hivi karibuni itadhihirika hata kwa wanaotupinga leo. Nasema tutarejea tukiwa imara, imara, tena imara, Inshaallah," alisema Manara.

Khalid Adam, Kocha Mkuu wa Mwadui FC, alisema kikosi chake kiko imara na kamili kuwavaa Simba huku kikiamini wana nafasi ya kuwaangusha mabingwa hao watetezi.

Kocha huyo alisema kila mchezaji wa Mwadui yuko tayari kuipigania timu ili kuvuna pointi tatu na wataingia uwanjani bila ya hofu.

"Tunajua wataingia na presha, wametoka kupoteza mechi mechi mfululizo, haitakuwa rahisi kwao kutulia, wakiruhusu kucheza kwa presha itawamaliza, nimewaambia wachezaji wangu wasiwe na haraka wanapokuwa na mpira, tutawamudu," Adam alisema.

Kocha Mkuu wa Yanga, Cedriz Kaze, alisema wamefika salama Musoma na wanachosubiri ni muda wa mechi ufike ili wakamilishe kazi iliyowapeleka mkoani humo.

Kaze alisema mechi zote za Ligi Kuu Bara ni muhimu na amewataka wachezaji wake kuzipa umuhimu unaofanana kwa sababu zitawasaidia kufikia malengo waliyonayo ya kuwavua watani zao ubingwa.

"Tuko salama, kila mchezaji alioko huku anasubiri mechi, ninajua Biashara ni timu nzuri kwa kuangalia rekodi zake, lakini Yanga pia ni timu kubwa na nzuri, tutafanya mbinu zetu ili kuhakikisha kesho (leo), pia tutapata pointi tatu," Kaze alisema.

Kocha Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, aliliambia gazeti hili amewaandaa wachezaji wake kwenda kupambana kusaka ushindi na si matokeo mengine ili kuendelea kujenga heshima kwenye uwanja wa nyumbani.

"Nimewaambia wakapambane na kila mchezaji atakayekuwa na jezi ya njano uwanjani bila kujali uwezo wake upoje ndani ya uwanja. Wakitulia na kucheza kama tulivyojipanga, Yanga haiwezi kupata pointi hata moja," Baraza alisema.

Aliongeza msimu huu amedhamiria kumaliza katika nafasi tatu za juu na ili afikie malengo anahitaji kushinda idadi nyingi ya mechi za mzunguko wa kwanza.

"Najua wamekuwa na ukuta mzuri, wamefungwa mabao machache ndani ya ligi, kwa sababu tunacheza nyumbani, naamini nafasi ya kuweka rekodi kwao ipo na inawezekana, tumewasoma na kuwafuatilia kwenye mechi zao zote, hakuna mabadiliko walivyoanza msimu na sasa wakiwa chini ya kocha mpya (Kaze)," Baraza aliongeza.

Yanga itaendelea kukosa huduma ya nyota wake wa kimataifa kutoka Angola, Carlos Carlinhos, Mapinduzi Balama ambao ni majeruhi na Haruna Niyonzima anayesumbuliwa na malaria. Azam FC yenye ndio vinara wa ligi hiyo na jana usiku walishuka dimbani kuwakabili JKT Tanzania.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya Prisons dhidi ya Polisi Tanzania wakati Namungo itawakaribisha Dodoma Jiji kwenye Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >